Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 11 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2009/2010.

Taarifa ya Sera za Fedha kwa Kipindi cha mwaka 2008/2009 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2009/2010.

## KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA , URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge kama ifuatavyo, chini ya kifungu cha 150 (1) cha Kanuni za kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa, Mkutano wa kumi na sita (16) wa Bunge wa kushughulikia Bajeti, pamoja na shughuli zingine za Bunge zilizopangwa, zimepangwa kufanyika kwa muda wa siku 38 tu; na kwa kuwa muda huu umepangwa kwa kuzingatia umuhimu wa kupunguza muda kutoka siku 50 uliowekwa na Kanuni ya 99 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 na kwa kuwa muda huu unapunguzwa kutokana na sababu za msingi zifuatazo:-

(1) Kuiwezesha Serikali kupitia Mamlaka yake ya Mapato *(TRA)* kuanza mapema kazi ya kukusanya Mapato na kutumia sheria mpya ya fedha itakayopitishwa na Bunge *(Financial Bill).*

(2)Kuleta mabadiliko ya mfumo na utaratibu wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa kuliwezesha Bunge kupitisha makadirio hayo kwa muda mfupi kutokana na kutoa nafasi kubwa kwa Kamati za Bunge za kisekta kupitia makadirio hayo kwa niaba ya Bunge kama inavyofanyika kwenye mabunge mengi ya nchi za Jumuiya za Madola, kama vile Australia, India, Afrika ya Kusini na Canada.

(3)Kuzingatia hali halisi ya Tanzania kuwa moja ya nchi zinazoathirika sana na kuyumba kwa uchumi wa Dunia kunakolifanya Bunge lizingatie hali hiyo na kuchukua hatua za kuiepusha Serikali kuingia kwenye gharama zinazoweza kuepukika.

(4)Jukumu kubwa la Bunge la kukamilisha maandalizi ya Mkutano wa 55 wa *CPA* utakaofanyika Arusha mwezi Septemba na Oktoba mwaka huu 2009.

(5) Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao mchakato wake unatarajiwa kuanza mwezi Agosti mwaka huu 2009.

Na kwa kuwa, baada ya kuzingatia sababu hizi za msingi, Kamati ya Uongozi imeweka utaratibu utakaorahisisha uendeshaji wa shughuli za Bunge mahsusi kwa ajili ya kupitisha Makadirio ya Mapato ya shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 yatakayowasilishwa kwenye Mkutano wa 16 wa Bunge hili yaani leo baadaye.

Na kwa kuwa ili kuwezesha utaratibu huo kutumika wakati wa kupitisha Makadirio hayo ni lazima Bunge litengue Kanuni kadhaa za Bunge zinazotumika kwa sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007.

Kwa hiyo, basi Bunge sasa linaazimia kwamba kwa madhumuni ya Bunge kupitisha Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Kanuni husika Toleo la 2007 zitenguliwe kama ifuatavyo:-

(1) Kanuni ya 99(6) inayoelekeza kwamba Waziri anapowasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake atatumia muda usiozidi dakika sitini utenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike; 'isipokuwa kwa hotuba ya Bajeti na Ofisi ya Waziri Mkuu muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini'.

(2)Kutengua Kanuni ya 99(7) inayofafanua kwamba Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio ya Wizara husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wanapotoa maoni yao watatumia muda usiozidi dakika 30 kila mmoja utenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike. Ninanukuu kanuni ndogo ya (7), "Waziri atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambao watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika 20 kila mmoja".

(3)Kutengua kanuni ya 99(9) inayoeleza kwamba Waziri mtoa hoja atapatiwa muda usiozidi dakika 60 kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike; Endapo Spika au Mwenyekiti ataona kuwa muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kwisha atafunga mjadala ili kumpa Waziri mtoa hoja nafasi ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge wakati wa majadiliano kwa muda usiozidi dakika 30.

(4)Kutengua kanuni ya 101(2) inayohusu mjadala katika Kamati ya Matumizi itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike; naomba kunukuu kanuni ndogo ya pili,

Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu lililohusika wakati wa kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.

Naomba kurejea kunukuu Kanuni ya (2), "Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu lililohusika wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi'.

Pia Kanuni ndogo ya (3) Mbunge atakayeomba ufafanuzi au maelezo kwa kutumia utaratibu huu ataruhusiwa tu iwapo anataka ufafanuzi au maelezo ya ziada kuhusu jambo linalohusiana na kifungu husika na si kwa jambo la jumla na hataruhusiwa kuomba ufafanuzi au maelezo ya ziada kuhusu mambo mawili kwa wakati mmoja isipokuwa kwa idhini ya Mwenyekiti.

(5)Mbunge aliyepewa idhini na Mwenyekiti chini ya fasihi ndogo ya (3) hapo juu hatazungumza zaidi ya mara moja juu ya jambo hilo.

(6) Aidha, pamoja na mapendekezo ya kutengua Kanuni zilizoorodheshwa hapo juu tunaleta pia pendekezo la kuongeza kipengele kipya cha Kanuni ya 146(3) kuhusu mavazi rasmi ya Wenyeviti wa Bunge wanapokuwa wanaongoza vikao vya Bunge, na mapendekezo ya kurekebisha Kanuni ya 146 (4) inayohusu mavazi rasmi Bungeni kwa Katibu wa Bunge na wasaidizi wake wanapokuwa kwenye ukumbi huu kama ifuatavyo:-

Vazi rasmi la Wenyeviti wa Bunge kuanzia sasa litakuwa ni Joho lenye kuonyesha michirizi ya rangi ya Bendera ya Taifa kulia na kushoto ya nembo ya Taifa katika mabega iliyoshonwa maalum kwa ajili hiyo ambalo litavaliwa juu ya vazi lolote ambalo ni vazi rasmi kwa Wabunge' Mheshimiwa Spika, Vazi rasmi la Katibu na Wasaidizi wake mezani litakuwa ni Joho la Rangi nyeusi lililoshonwa maalum kwa ajili hiyo ambalo litavaliwa juu ya vazi lolote ambalo ni vazi rasmi kwa Katibu na Wasaidizi wake Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo ya kubadili Kanuni na pia kuweka Kanuni ya ziada kuhusu mavazi rasmi kwa Wenyeviti na Katibu na Wasaidizi wake, imekwishatolewa na imeungwa mkono. Niongezee tu kwa nafasi hii kwamba baada ya mazungumzo yetu kwenye *Brifieng* tumefanya mabadiliko katika Kamati ya Uongozi kwa kuzingatia maoni yenu Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha itajadiliwa kwa siku nne (4) badala ya tatu. Hoja ya Waziri Mkuu nayo itajadiliwa kwa siku nne(4) badala ya tatu na uchangiaji utabaki vilevile dakika kumi na tano na siyo kumi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo tunaendelea na shughuli zinazofuata. *(Makofi)*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri Mkuu, Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 pamoja na mabadiliko mbalimbali yaliyofanyika. Katika Sheria hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu haki ya raia kupiga kura kwanza ni kuwa Raia wa Tanzania awe ametimiza miaka 18 na asiwe mwendawazimu. Ni sheria ipi inayotumika kwa Raia waliopo Zanzibar kukataliwa kuandikishwa kwa sababu tu hawana vipande vya ukaazi wakati Sheria ya Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina sharti hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu hii ina pande mbili za Muungano, upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na tunao vilevile upande wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ina mambo yanayoingiliana kwa pande zote mbili lakini yapo mambo mengine ambayo yanasimamiwa na taratibu za ndani ya kila pande. Ameuliza kitu kinaitwa kipande mimi sijui kipande ni nini. Lakini inawezekana kwa utaratibu wa Zanzibar ni jambo ambalo pengine wameliweka kwa lengo la kuweka ufanisi katika Uchaguzi. Lakini inaonekana pengine ni jambo linahitaji kutazamwa zaidi nadhani ni juu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuliangalia na kuona kama inaweza likaboreshwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, tunachozungumzia ni Katiba na Sheria. Nchi yetu inaheshimu utawala bora na kwenye utawala bora moja ni kuheshimu haki ya raia na haki ya raia ni kuchagua na kuchaguliwa ni moja kati ya haki ya msingi ya raia. Huu utaratibu unaovunja sheria na Katiba. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaweza tukaruhusu Katiba ya Nchi au sheria za nchi zivunjwe tu kwa sababu ya mazingira ya pahala?(*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema kama inaonekana ni jambo linalohitaji kutazamwa basi ni vizuri jambo hili tukaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili iangalie ili waone kama kuna maeneo tunaweza tukafanya marekebisho ili kuweza kuzingatia jambo hilo.

Lakini kama unaona ni jambo kweli linahitaji kutazamwa kwa upande mwingine hakuna ubaya unaweza ukaleta hoja pengine nzuri tukaitazama kwa maandishi tuone hasa *details* zake zinasema nini halafu sisi tunaweza tukawasiliana na wenzetu tuone wanatuambia nini.(*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika naomba kumwuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali lifuatalo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1996 Serikali ya Tanzania ilitangaza rasmi kuhamisha wakazi wa Kipawa ili kuruhusu upanuzi wa Uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, sambamba na uamuzi huo Serikali vilevile ilitathmini nyumba zote ambazo ziko pale zinazokadiriwa kuwa 1,300 na baadaye ilitoa uamuzi wa kulipa fidia kwa nyumba hizo, lakini kubwa zaidi ni kuwa Serikali ilitoa amri kuwa wamiliki wote wa nyumba zile hawaruhusiwi kuendelea kujenga wala kufanya ukarabati wa aina yeyote.

Mheshimiwa Spika, toka uamuzi huo wa Serikali kutolewa ni miaka 12 sasa wananchi wa Kipawa hawajalipwa fidia yeyote na wanaendelea kuishi katika maisha ya taabu na katika nyumba ambazo hata binadamu wa kawaida hawezi kuishi.

Je, kwa kuwa hawa wamekaa muda mrefu kutekeleza wito wa Serikali au amri ya Serikali ya kuwa wasijenge. Sasa kwa sababu hawa wameshindwa kujiendeleza ni lini Serikali itawapa fidia yao ili waweze nao kujiendeleza?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolieleza Mheshimiwa Khamis ni kweli kwamba Serikali ilifanya maamuzi hayo lakini ni kweli vilevile kwamba imechukua muda mrefu kuweza kuyatekeleza kutokana na sababu mbalimbali, lakini bado ni dhamira ya Serikali kwamba jambo hili litamalizika muda si mrefu.

Hivi karibuni tulikuwa tunajaribu kufanya mazungumzo na Serikali ya China katika kujaribu kutimiza hiyo ahadi ya kujaribu kuboresha uwanja wa ndege lakini wakati huo huo kuchukua hatua ya kufidia wale wote ambao tulikuwa tumeona ni vizuri wakapisha ili tuweze kupanua uwanja ule wa ndege.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niamini kwamba wakati Waziri wa Miundombinu atakapokuwa anawasilisha Bajeti yake jambo hili atalieleza ili wananchi waweze kujua hasa ni jambo gani tumekubaliana maana hata mimi silipendi ni kitu ambacho kinakera lakini tulilazimika kufika hapo. Lakini nadhani sasa tupo kwenye hatua nzuri zaidi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, wakati tathmini zilipofanywa mwaka 1996 hadi leo kuna mabadiliko makubwa na inawezekana kwamba bei zile hazilingani na hali halisi. Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini mpya ili kuendana na wakati?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika ni kweli kwamba muda umepita na umekuwa mrefu kidogo lakini mimi siwezi kujibu haraka haraka hilo ulilotaka niliseme ndiyo maana nimesema kwa sababu Waziri wa Miundombinu atakuwa na jambo hili kwenye Bajeti yake nina hakika hilo litakuwa limezingatiwa kama watafanya tathmini au pengine wameshafanya tathmini kwa namna fulani ya kuongeza kwa asilimia jambo kama hilo. Nadhani atakuwa kwenye nafasi nzuri sana ya kuwaeleza Watanzania ili waweze kujua hali halisi sasa ikoje.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali lifuatalo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kesi zinazoendelea hapa nchini sasa hivi za watuhumiwa wa ufisadi pamoja na watuhumiwa wa wizi wa hela za *EPA*, ni *very high profile cases*, ambazo zimevuta hisia kubwa sana za Watanzania. Kwa nini Serikali haishauriani na Mahakama ili waunde mahakama maalum kwa kutumia Mahakimu maalum wenye *very high integrity* ili kesi hizi ziendeshwe haraka na kumalizika kama ilivyofanya kwa watuhumiwa wa mauaji ya albino ili nchi yetu iachane na wimbo huu mbaya tuendelee na wimbo wetu wa kutafuta Maisha Bora kwa kila Mtanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametumia mfano wa kesi za mauaji, siwezi mimi nikaita kwamba ile ni Mahakama Maalum, hapana! Tulichofanya pale ni kuweka utaratibu unaowezesha kusikiliza kesi kwa haraka kwa sababu Mahakama zilivyokaa wakati mwingine zinatumia mtindo ule wa *session* kwamba inabidi ungoje mpaka mwezi fulani au mpaka muda fulani mpaka kesi zifikie idadi fulani ndiyo muweze kufanya ile *session* ya Mahakama Kuu.

Kwa hiyo, tulimwomba Jaji Mkuu hizi kesi hata kama ni mbili ama tatu tunaomba ziendelee lakini kwa kweli Majaji utaratibu wao ni ule ule. Upande wa kesi hizi ambazo anazizungumza ni utaratibu wa kawaida. Hakimu yupo na Mawakili wapo Dar es Salaam wanaendesha kesi zile kulingana na maelewano kati Mawakili upande wa Serikali Kuu na upande wa Mshtakiwa. Kwa hiyo, hakuna umaalum ambao kwa kweli ujengwe *unless* kama labda ulitaka kusema jambo fulani maalum ambalo sikulielewa vizuri sana. Lakini utaratibu ule ni suala tu la kuomba pande zote mbili zitoe msukumo kwenye kesi hizo ili mtu asipate kisingizio kwamba shahidi mmoja hayupo au Wakili leo anaumwa, kwa sababu hilo jambo litaendelea hata kama utasema uiite maalum lakini bado kama Wakili hayupo hayupo. Kwa hiyo, mimi nadhani ni suala tu la kuiomba Mahakama na Serikali kwa maana ya waendesha mashtaka kuchukua jambo hili kwa uzito unaotakiwa ili kupunguza visingizio vinavyojitokeza wakati wa kuendesha kesi.

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wakati wa Uchaguzi Mkuu Tanzania pamoja na chaguzi nyingine ndogo, kunatokea malalamiko mbalimbali kutoka Vyama vya Siasa kuhusu baadhi ya watu ambao huwa wanathubutu kupiga kura mara mbili au zaidi pamoja na sheria zilizopo; na kwa kuwa Zanzibar kuna vitambulisho au *ID* ambazo inasemekana ni za kisasa zaidi zenye mfumo kama huu?

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha aina ya vitambulisho alivyokuwanavyo).*

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Lakini nchi nyingi za Afrika pamoja na Afrika ya Kusini, vitambulisho vilivyopo ni vitambulisho ambavyo vinaweza kuwekwa kumbukumbu tofauti sawa na vile vitambulisho vilivyotolewa Zanzibar miaka ya 1970 vyenye mfumo kama huu?

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha tena aina ya vitambulisho alivyokuwa navyo)*

**MHE: MOHAMED HABIB MNYAA:** Vitambulisho ambavyo mara nyingi sana Afrika ya Kusini na nchi nyingine wanazitumia *ID* hizi hata wakati wa kupiga kura ambapo Tume ya Uchaguzi inakuwa na sehemu ya kupiga mhuri kitu ambacho kinasaidia kudhibiti mtu asiweze kupiga kura mara mbili.

Je, katika mpango wa Tanzania *ID* zinazotaka kutolewa zitakuwa na mfumo gani ambao unaweza ukaruhusu kuweka kumbukumbu na tukaweza kuzitumia katika shughuli tofauti au, mfumo kama huu wa Zanzibar ambao hauna sehemu ya kuweka kumbukumbu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, swali lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Vitambulisho vya Kitaifa ambavyo vinatarajiwa kutumika hapo baadaye, bado liko kwenye mchakato, halijakamilika. Ukiniuliza mimi nitasema sijui kama itafanana na hicho cha Zanzibar au hapana. Ninaloweza kukuhakikishia tu ni kwamba, mfumo ambao utaingizwa kwenye hicho kitambulisho ni mfumo ambao kwanza, tulitaka uwe kiusalama si kitambulisho ambacho mtu yeyote anaweza akacheza nacho kukibadili au kukigeuza kutumika kwa njia ambazo siyo halali. Kwa hiyo, suala la usalama wa hicho kitambulisho kwa maana ya kuepusha uwezekano wa watu kuvitumia vibaya, litazingatiwa. Lakini la pili, ni kwamba tungependa vilevile vitambulisho hivyo kwa sababu tuko katika

karne ya 21 kwa kadri itakavyowezekana viwe ni vitambulisho vinavyoweza kutumia vilevile mifumo mingine mingi zaidi kuliko kuwa tu ni kitambulisho.

Masuala ya kodi, masuala mengine yanahusiana pengine hata uchaguzi kama unavyosema, yanaweza kuwa ni baadhi ya mambo ambayo yatakuwemo katika hicho kitambulisho lakini siwezi nikakuhakikishia moja kwa moja mpaka mchakato utakapokuwa umefikia hatua sasa ya kuweza kuanza kuanisha kitaambulisho hicho kina *features* za namna gani au sura ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, lakini nadhani rai yake ya msingi kwa Serikali hapa ni kwamba, ni vizuri kitambulisho hicho mjitahidi kiweze kuwa na mifumo itakayoruhusu mambo mengi badala ya kukaa tunategemea mifumo mingi kwa wakati mmoja. Mimi nadhani hilo ni jambo jema na ni jambo ambalo linastahili kuzingatiwa.

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa jibu zuri sana alilonipa Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini sasa labda swali la nyongeza ni dogo. Ili kukuza demokrasia yetu na Tanzania kupata heshima zaidi, je, inaweza ikafanyika huu mchakato unaoendelea hivi sasa ambao hujaujua uko vipi, unaweza ukaharakishwa ili tukaweza kuvitumia vitambulisho hivyo katika Uchaguzi wa 2010 (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi na Mheshimiwa Mnyaa wote tunatamani iwe hivyo, kwa sababu kwa kweli ndio dhamira hasa ya Serikali. Na matarajio yangu kwamba bado tutajitahidi kuendelea na mtazamo huo lakini usije baadaye tena ukasema nilisema, ninachosema ni matazamio yangu kwamba lengo liwe ni hilo. Lakini kunaweza kukatokea jambo lolote hapo katikati kwa sababu ni mchakato pengine mkashindwa, tukachelewa, lakini tutajitahidi kuona kama tunaweza tukatimiza azma hiyo njema. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, *Law School;* Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kwa vipindi kadhaa iliwahi kutoa ahadi ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa *Law School* lakini pamoja na ahadi hiyo, haijawahi kutekelezeka hata mara moja. Hivi ninavyozungumza mimi mwenyewe niliwahi kufika kwako na ukaniahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba suala hilo litatekelezwa na utalishughulikia wewe mwenyewe lakini halijatekelezwa, na hapa ninapozungumza wako wanafunzi wamesimamishwa hawaendelei na masomo kutokana na tatizo hilo.

Je, Serikali inatoa tamko gani kumaliza tatizo hilo moja kwa moja? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Killimbah kidogo amenionea, baada ya kuwa ameniomba mara ya kwanza, angekuja kuniuliza tena kusema wewe Mheshimiwa hivi umefikia wapi ningefarijika sana. Kwa sababu Serikali si kwamba haijafanya lolote kwenye suala la wanafunzi wale ambao wanasoma katika Shule ya Sheria *(Law School*), jambo hili lililetwa Serikalini nimelisimamia mwenyewe tukakaa na Hazina na tukatoa karibuni kiasi cha shilingi Bilioni moja kwa ajili ya kulipa fedha za wanafunzi wale na zoezi hilo likafanyika. Sasa kilichojitokeza ni matatizo ya utekelezaji.

Baadaye tumegundua kwamba katika zoezi lile wako wanafunzi ambao walistahili kulipwa kihalali na wengine ambao hawakustahili. Hawa ambao hawakustahili na wenyewe wamefaidika na huo utaratibu, matokeo yake ni kwamba baadhi ya wale waliostahili wamekosa kupata zile fedha ambazo walistahili kupata. Kwa hiyo, hilo ndilo jambo ambalo tunajaribu kulisawazisha, tukiishalimaliza tunaamini tutafika mahala pazuri ili na hao

wanaolalamika wachache tuweze kuwamaliza vilevile. Lakini juhudi imefanyika na tulifanya kwa dhamira nzuri sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Waziri Mkuu zoezi zima la kuwaondoa wafugaji kwenye maeneo ya wakulima. Moja katika tatizo lililompata ndugu yangu Clement anayeishi katika Kata ya Mkande Jimbo la Solwa ni kwamba alipoteza ng'ombe 52. Kwa bahati nzuri ameziona ng'ombe hizo kwa Mzee Maberu anayekaa Kijiji cha Ngagala Mkoa wa Tabora. Mheshimiwa Waziri Mkuu unamsaidiaje huyu apate ng'ombe wake?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili ni kinyume cha Kanuni kwa sababu ni swali mahususi ambalo lingeweza kushughulikiwa na Serikali kupitia Waziri tu anayehusika. Ningemshauri Mheshimiwa Mbunge amwone Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kupata ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali yamekwisha kabla ya dakika 30 nakushukuru sana. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 20

### Uthibiti wa Dawa Feki kwa Matumizi ya Binadamu

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inawajibika kutengeneza mazingira mazuri ya kuwalinda wananchi wake dhidi ya dawa feki zinazouzwa kwenye maduka nchini na kwa kuwa yapo maduka yanayouza dawa zilizo chini ya viwango.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo na kama inafahamu kuwa tatizo hili lipo limesababishwa na nini?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kudhibiti tatizo hilo la dawa zilizo chini ya viwango vinavyotakiwa?

(c) Je, ni athari zipi zinazoweza kupatikana kwa kutumia dawa hizo zisizokidhi viwango vya matumizi kwa binadamu kwa mfano dawa feki ya *Metakelfin?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifautavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu tatizo la kuwepo kwa dawa feki (bandia) kwenye maduka ya dawa nchini na vile vile kuwepo kwa maduka yanayouza dawa zilizo chini ya viwango. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa linasababishwa na watengenezaji wa dawa wasio waaminifu pamoja na wafanyabiashara wenye uchu wa utajiri wa haraka wanaoingiza dawa hizo kwa lengo la kupata faida kubwa. Mambo mengine yanayochangia urahisi wa

kuingiza dawa bandia ni pamoja na mfumo wa biashara uliopo wa soko huria na vile vile nchi yetu inapakana na nchi nane hii inapelekea uwepo wa njia nyingi zilizo rasmi na zisizo rasmi (njia za panya).

(b) Mheshimiwa Spika, katika kupambana na dawa bandia nchini, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya chakua na dawa na wadau wengine imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuwapatia mafunzo wakaguzi wa dawa juu ya namna ya kutambua dawa bandia na zile zilizo duni.

(ii) Kuweka wakaguzi wa dawa mipakani ambapo mpaka sasa kuna kaguzi katika vituo 11 vya forodha vinavyoingiza dawa nchi nzima.

(iii) Kufanya operesheni maalum za kushtukiza kubaini dawa bandia kwa kushirikiana na taasisi nyingine na vyombo vya ulinzi na usalama yaani Jeshi la Polisi, mamlaka ya mapato, Tume ya ushindani, shirika la viwango, Ofisi ya Rais Usalama wa Taifa na mtandao wa polisi wa kimataifa (*Interpol*).

(iv)Tatizo la dawa bandia linazikumba nchi hizo duniani kwa hiyo, nchi yetu inashirikiana na mataifa mengine katika kupambana na dawa hizo bandia. Pia ufuatiliaji wa ubora na usalama wa dawa zilizopo sokoni na kufanya uchunguzi wa kimaabara.

(v)Kutoa elimu kwa umma juu ya dawa feki kupitia vyombo vya habari nchini kama vile televisheni, radio na magazeti.

(vi) Kuimarisha maabara ya mamlaka ya chakula na dawa kwa kuweka vifaa vya kutosha na vya kisasa vyenye uwezo wa kupima na kubaini ubora wa dawa na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wachunguzi. Vile vile mamlaka imeweka maabara ndogo nane zinazohamishika katika vituo vya mipakani na hospitali za mikoa, mashine hizi hutumika kupimia ubora wa dawa zinazoingia na kutumika nchini.

(vii)Kuundwa kwa kikosi kazi baina ya *TFDA* na Jeshi la Polisi chenye jukumu la kupanga mikakati ya pamoja na kufanya operesheni za kutafuta na kukamata dawa bandia na duni kwa kushirikiana na wadau wengine.

(c) Mheshimiwa Spika, athari zinazoweza kupatikana kwa kutumia dawa bandia au zisizokidhi viwango mfano dawa feki ya *Metakelfin* ni kama ifuatavyo:-

(i)Kwa kuwa mgonjwa hatapata dawa halisi ugonjwa wake unaweza kuendelea hivyo kumpa madhara na pengine kusababisha kifo.

(ii)Utumiaji wa dawa ambazo dozi yake ni ndogo ndiyo mwanzo wa kusababisha usugu wa vimelea kwa dawa.

(iii)Dawa zisizo na ubora unaotakiwa zinaweza kuwa na sumu ambazo zinaweza kusababisha madhara ya kiafya kama ulemavu na hata vifo.

(iv)Kusababisha hasara kwa Serikali au mtu binafsi kwa kununua dawa zisizo na viwango (*value for money*).

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri na jitihada nzuri makini za Wizara katika kudhibiti madawa haya yasiyokidhi viwango hivi leo tunaona matatizo yote haya.

(a) Je, Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kutathimini jitihada hizo za kudhibiti madawa haya kwa mara nyingine ili kuzuia vifo vya Watanzania?

(b) Waziri atakubaliana kushirikiana nami kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa kutoa elimu kwa wananchi wa Mkoa huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimejibu katika jibu langu la kwanza yote ambayo tumeyafanya haya ni kutokana na tathimini na kuona kwamba ni jinsi gani dawa hizi ambazo zina ubora hafifu zinaingizwa nchini mwetu.

Lakini nakubaliana kabisa kwamba kuna umuhimu wa kufanya tathimini ya ziada ili kuweza kuhakikisha kwamba dawa hizi zinaweza kudhibitiwa zaidi ili wananchi wengi wasiweze kuathirika.

Kuhusu kutoa elimu kwa Mkoa wa Iringa, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali inatoa elimu kupitia vyombo vya habari. Lakini vile vile katika maeneo ya Mikoani kama nilivyosema tunao viongozi ambao tunashirikiana sana na TAMISEMI ambao wanatakiwa wawe wanatoa elimu na ukaguzi wa hapa na pale katika haya maduka ambayo wanauza dawa hizi feki.

Lakini vile vile siwezi nikamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kwenda kumtolea lakini tukipata nafasi basi tunaweza tukaleta watalaam na kwenda kuwafahamisha wananchi wa Iringa na wananchi wengine ili iweze kujua na kuzigundua zile dawa feki ili zisije zikaleta madhara zaidi. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kipindi cha Bunge kinapokuwa kimeanza mara nyingi dawa nyingi zinakuja hapa Bungeni hasa za asili na kwa kuwa Wabunge wengi wanapozitumia wanapata kizunguzungu wengine inabidi wapumzike. Je, Wizara haioni kwamba Wabunge kuendelea kutumia dawa hizi wanaweza wakapata matatizo ya afya zao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na tabia wakati tunapokuwa Bungeni watu wengi tunawaona wakiwa katika maeneo ya Bunge wakiwa wanakuja hapa kutoa dawa ambazo zinaitwa dawa za asili. Ukweli ni kwamba sisi tumeliona hili kama Wizara tumekuwa tukilifuatilia lakini tumeambiwa kwamba wao wanapata kibali kutoka Ofisi yako Mheshimiwa Spika. Sisi Wizara ya Afya tulikwenda pale tukaona na tukawaambia kwamba marufuku wasije lakini tukaona tena kwamba wao wakileta dawa zao hapa huwa hawapati ruhusa kutoka Wizara yetu. Sisi kama Wizara tumeweka pale zahanati ambayo hii ina watalaam.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nilitaka kuwaomba ni kwamba kama kuna mtu ana tatizo aende zahanati ili aweze kupata ushauri lakini wale wanaokwenda kupata dawa ambazo sisi kama Wizara hatukuziafiki na wala hatukuzipitisha kuja hapa Bungeni kwa kweli itakuwa ni vigumu sana kutoa jibu la hapa na pale. Lakini tutaendelea kufuatilia tuona kwamba wale

walioleta dawa zao wamepata kibali kutoka wapi ili tuweze kuona tunachukua hatua gani? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jukumu la Ofisi ya Katibu wa Bunge ni kutoa fursa pamoja na fursa mbadala kwa Waheshimiwa Wabunge. Wapo Wabunge wengi sana wanaoamini katika dawa za aina hiyo.

Sasa isingekuwa vema tukazuia kwa sababu hatuna taarifa kwamba dawa hizi zimezuiwa kwa nchi nzima. Kwa hiyo, biashara inayoendelea pale ya magazeti ya vitu vingine ni kutoa fursa tu ili Mbunge ambaye anayependa dawa mbadala basi aweze kufaidika. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi la kuhusu maduka yanayouza dawa ambazo zina athari kubwa ya kuua wananchi wa Tanzania.

Je, kama Serikali sijaona mkakati wowote ambao wanaweza kunieleza sasa wanawajibikaje hawa wenye madawa ambao wanauza na wanawajua kabisa haya madawa yamepigwa marufuku, Serikali imejipangaje?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya kwa kupitia *TFDA* na vyombo ambavyo nilivitaja katika jibu langu la msingi ni kwamba kama nilivyosema tumekuwa tukifuatilia na kufanya ukaguzi wa kustukizia na kama wote mtakuwa mnaona Waheshimiwa Wabunge ni kwamba wale ambao wanakamatwa zile dawa zinachukuliwa lakini wale wananchi wanapelekwa katika vyombo vya sheria na sheria inachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ili kuliona hili sasa sisi kama Wizara tumeanzisha maduka ya dawa muhimu ambayo yanaitwa *ADO* ambayo nadhani Mheshimiwa Waziri baadaye atakapokuja kuwasilisha Bajeti yetu yake ataelezea vizuri ni kuhakikisha kwamba hata kule katika maeneo ya vijijini wananchi watapewa elimu ambayo wale wenye maduka ya dawa muhimu watakuwa na elimu zaidi ya kuweza kujua hii ni dawa feki au ni dawa gani ili wanapokuwa wanauza dawa zao zile ambazo ni karibu na wananchi waweze kuwahudumia vizuri na kuweza kuzitambua kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

Na. 21

**Kurekebisha Hati na Kuendeleza Mashamba Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikubali kuwapatia makazi mapya na mashamba wananchi waliopewa fidia ili kupisha hifadhi ya Msitu wa Derema. Tarafa ya Amani, Muheza na kwa kuwa, baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza lilipitisha azimio ambalo liliungwa mkono na Kamati ya Maendeleo ya Mkoa la kutaka hati za mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa ya *Kibaranga Estate, Bwembera Estate, Kumburu Estate, Lewa Estate, Kihuhwi Ruber Plantation* na *Azimio Ranch* kufutwa au kumegwa maeneo yake ili wananchi wenye shida ya ardhi wapewe.

(a)Je, ni lini marekebisho ya hati hizo yatafanyika ili wananchi wa Derema, Amani na wale wenye shida ya ardhi katika maeneo ya jirani wapate ardhi?

(b)Je, Serikali haioni haja ya kukutana na wadau ili kupanga upya umiliki na uendelezaji wa mashamba hayo ili kutatua migogoro ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji wapya?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninge kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi Mbunge wa Muheza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Benki ya Dunia ilitoa fedha kuwafidia wananchi waliokuwa wanaishi katika msitu wa Derema ambao kwa sasa ni Hifadhi ya Msitu kwa masharti kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Muheza iwapatie ardhi mbadala wananchi hao. Halmashauri iliahidi kufanya hivyo lakini ahadi hiyo haijatekelezwa mpaka sasa.

Aidha, mapema mwaka huu 2009 wawakilishi wa Benki ya Dunia walipofuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo hatimaye suala hili lilifikishwa katika kikao cha Kamati ya Mashauriano ya Mkoa wa Tanga (RCC) ambapo kikao hicho kiliagiza kwamba hatua za kufuta miliki za mashamba ya Mkonge ambayo hayajaendelezwa zichukuliwe haraka. Mashamba hayo ni *Kibaranga Estate*, *Bwembera Estate, Kumburu Estate, Lewa Estate, Kihuhwi Ruber Plantation* na *Azimio Ranch*.

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeanza kutekeleza agizo hilo kwa kutoa ilani ya kufuta miliki ya shamba la Kibarangu; Ilani hiyo ilitolewa tarehe 14 Mei, 2009 na Wizara yangu imepata nakala.

Muda wa notisi utakapomalizika baada ya siku 90 Halmashauri ya Muheza ilileta rasmi Wizara kwangu ombi la kufuta miliki hiyo na Wizara yangu itawasilisha ombi hilo kwa Mheshimiwa Rais ili miliki hiyo ifutwe kwa mujibu wa sheria.

Marekebisho ya hati husika yatafanyika baada ya kukamilika ufutaji wa miliki ya shamba hilo ili wananchi wa Derema, Amani na wengine katika maeneo ya jirani wenye shida ya ardhi waweze kupata ardhi itakayomegwa kutoka katika shamba hilo.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu wa kukaa na wadau ili kusuluhisha migogoro ya ardhi inapotokeza. Hivyo kwa kuzingatia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Wizara yangu inashauri Viongozi wa Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Muheza wakae na wadau na kuzungumza jinsi ambavyo wanaweza kupata ufumbuzi wa tatizo la uhaba wa ardhi linalowakabili wananchi katika Mkoa wao. Nia iwe kuwapatia wananchi ardhi kutoka kwenye mashamba makubwa yaliyotekelezwa ili waweze kujiendeleza.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, wawakilishi wa Benki Kuu wanaye mwakilishi wao hapa Tanzania na taarifa ambazo nimezipata siku mbili zilizopita zinaonyesha kwamba wawakilishi hawa hawajaridhika sana na jinsi taratibu hizo zitakavyochukuliwa hasa zinavyokwenda taratibu.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri haoni ipo haja ya kuchukua hatua za dharua za kutoa hekta 921 kutoka shamba la Kibaranga ambalo tayari zimekwishapimwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili wananchi wale waweze kupatiwa na tuondokane na migogoro na Benki ya Dunia wakati taratibu nyingine zikiendelea?

(b) Kwa kuwa baadhi ya viongozi wa Bodi ya Mkonge pamoja na hawa *consolidated Holding Company* wanaendelea kugawa mashamba haya hasa hili la Kibaranga na lile la Bwembera kwa wawekezaji mashamba ambayo tayari ndani ya baraza la Madiwani wa Wilaya ya Muheza wamekwishaomba hati zake zifutwe wao wanaendelea kuyagawa hata bila kuwashirikisha viongozi. Hawamshirikishi Diwani wa eneo, hawashirikishi Wabunge, hawamshirikishi hata Mkuu wa Wilaya. Je, Waziri anasema kuhusu hatua hiyo ambayo sisi haturidhiki nayo na tunaiona kama ni kichocheo cha migogoro kati ya wananchi na Serikali yao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza kwamba utaratibu unakwenda pole pole sana kwa hiyo Wizara ichukue hatua za dharura. Jibu ni kwamba inawezekana kweli kuna ucheleweshaji maana yake tangu walipokubaliana mwaka 2003 kati ya Benki Kuu na Halmashauri ya Muheza ni miaka karibu mitano, sita imeshapita.

Lakini kwa sasa hivi maadam sasa wameshaanza mchakato wa kutoa Ilani hatuwezi kukwepa ule mkondo wa sheria. Ilani kwa kawaida ni siku 90, siku 90 zikiisha za Ilani Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wataleta ombi sasa rasmi la kufuta hiyo ardhi Wizarani kwangu ninachoweza kumwahidi ni kwamba Wizara yangu ikishapokea ombi hili itafanya haraka kupeleka kwa Rais kwanza mimi pale sina siku hawa wenzangu wana siku 90, ninachotuma kwa hili ni kwamba ikifika Wizarani kwangu nitafanya haraka kumpelekea Mheshimiwa Rais ili ifutwe kwa mujibu wa sheria. Lazima tufuate mkondo wa sheria.

Kuhusu *consolidated Holding* kuendelea kuuza baadhi ya sehemu za mashamba kwa sasa hivi hawa ndio wenye hati miliki ndiyo wenye mali mpaka hapo tutakapofuta. Kwa hiyo, maadam wao ndiyo wenye mali huwezi kumzuia mtu mwenye mali yake kukodisha au kuiuza ni mwenye mali.

Tunachoweza tu ni kuwashauri kwamba wajue kwamba Serikali iko katika mchakato wa kufuta hizo hati miliki. Kwa hiyo, hizo harakati zao wanazozifanya waziache ni kuwashauri kwa sababu baadaye tukishafuta maana yake ni kwamba hata huyo aliyeuziwa atakuwa ameuziwa kitu batili.

Na. 22

**Kivuko Kipya Mto Ruhuhu**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeleta kivuko cha kisasa mto Ruhuhu; na kwa kuwa kivuko hicho kinashindwa kufanya kazi kutokana na kasi ya maji ya mto huo wakati wa masika, na kushindwa kufanya kazi wakati wa kiangazi kutokana na kina kifupi.

Je, Serikali haioni haja ya kujenga daraja mbadala litakalounganisha mikoa ya Ruvuma na Iringa kwenye sehemu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mbunge Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa kivuko cha kisasa cha tani 50 cha mto Ruhuhu kinachofanya kazi kati ya Kipingu (Ludewa) na Lituhi (Mbinga), kilianza kazi Novemba 2007 na kilinunuliwa kutokana na ahadi za Viongozi wa Kitaifa walizotoa wakati wa kampeni za Uchanguzi Mkuu wa Mwaka 2005 kwa ajili ya kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wa maeneo hayo.

Kivuko hiki kilinunuliwa kubadilisha kivuko cha zamani cha tani saba (7) kilichokuwa cha kamba kwa kutumia nguvu za wanadamu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa kutokana na kasi ya maji ya mto wakati wa masika na kupungua kwa maji wakati wa kiangazi kivuko hicho wakati mwingine hushindwa kufanya kazi.

Lakini pia nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kuwa suluhisho la kudumu la kuondoa kero hiyo ya usafiri katika eneo hilo ni kujengwa daraja la kuunganisha sehemu hizo mbili za mikoa ya Ruvuma na Iringa.

Hata hivyo kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha; hatua hii ya kuwa na kivuko ni suluhisho la muda ambalo tunatakiwa tuendelee nalo. Na ndiyo maana kwa hivi sasa Wizara yangu kupitia wakala wake wa Barabara (*TANROADS*), inafanya matengenezo ya maegesho ya kivuko hicho yaliyoharibiwa na mvua upande wa Lituhi (Mbinga) ili kivuko hicho kiendelee kufanya kazi ipasavyo. Na wakati huo huo naomba kutoa mwito kwa wananchi wote wanaoishi kandokando ya mto Ruhuhu kutunza mazingira ili mto huo uendelee kuwa na maji ya uhakika wakati wote wa mwaka kuwezesha kivuko kufanya kazi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya kuwezesha kupanga mpango wa kujenga daraja katika eneo hilo kwa siku za usoni.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kwanza Kampteni Komba ameniomba niwasilishe salamu zake za pongezi na shukrani kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wake wa Lituhi na wale Prof. Mwalyosi kule Ludewa kwa Serikali kuwajali na kuwanunulia kivuko kipya. Lakini kutokana na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ametujibu, haionyeshi kama kuna *commitment* yoyote ile ya kuona kwamba huu utaratibu wa kujenga daraja unafanyika.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwahakikishia wananchi wa Lituhi na Ludewa kwamba katika mpango wa mwaka ujao, mpango wa daraja utakuwemo?

(b) Ziko habari kwamba dereva anayeendesha kivuko hiki ni kama kibarua tu hajaajiriwa kwa mkataba wa kudumu na anamiliki chombo chenye gharama kubwa sana, Serikali ina mpango gani wa kumwajili dereva huyu kama hizi habari ni za kweli?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa niaba ya Serikali nipokee shukrani za Mheshimiwa Mbunge wa Mbinga Magharibi ambazo zimewasilishwa hapa na Mheshimiwa Kayombo, tunashukuru na kama nilivyosema katika

jibu la msingi hapa Serikali itaendelea kuwajali wananchi wake katika maeneo mbalimbali katika kutatua kero za usafiri. Sasa kwenye swali Mheshimiwa Mbunge angependa kama kuna *commitment* yoyote ambayo ni thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikutoa *commitment* yoyote thabiti hapa kwa sababu zile zile nilizozieleza katika jibu la msingi ya kwamba kwa sasa hivi Bajeti ya Serikali hairuhusu kutuwezesha kujenga daraja katika eneo hili. Lakini *commitment* ambayo nimeitoa ya jumla ni ile tu ya kwamba Serikali itaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha zitakapopatikana hapo kutakuwa sasa na nafasi nzuri ya kuweza kutoa taarifa rasmi kwamba ni lini daraja litaanza lakini kwa mwaka ujao nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kuwa na subira tutupie kivuko hiki kipya na wananchi wakifurahie tu na hapo baadaye fedha zitakapopatikana suala la daraja linaweza likaja.

Kuhusu suala la dereva ambaye ni kibarua kwa hivi sasa nataka niseme tu kwamba hili nimelipokea tutalifuatilia na kama lina ukweli kama yeye mwenyewe alivyosema kwamba amelisikia tu na sisi kama tutathibitisha kwamba habari hizo ni za kweli tutafanya marekebisho haraka iwezekanavyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru vilevile kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, niulize swali la nyongeza kwamba kwa vile kuna mradi mkubwa wa umwagiliaji unaohusisha hekta 3000 upande wa Mbinga na Ludewa kwenye eneo hilo ambako kuna kivuko na kwa vile ili kuwezesha mradi wa *irrigation* ufanye kazi vizuri unahitaji bwawa kubwa la maji kwa kujenga ukuta kwenye mto Ruhuhu ambao vilevile ingeweza kuwa ni daraja la kuvuka mto huo.

Je, Mheshimiwa Waziri akanithibitishia kwamba yeye upande wa Wizara ya Miundombinu anaweza kushirikiana na Wizara ya Umwagiliaji kuangalia kama wanaweza wakashirikiana kujenga tuta hilo ambalo inaweza kuwa ni daraja na tatizo na *solution* ya kudumu katika mto Ruhuhu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, kwa kututaarifu uwezekano wa ujenzi wa bwawa hilo ambalo anasema kwamba linaweza likawa suluhisho katika eneo hilo ambalo linahusisha masuala ya umwagiliaji. Lakini kama alivyopendekeza yeye mwenyewe kwamba bora tushirikiane na wenzetu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, nataka tu niseme tu kwamba Serikali ni moja tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa Wizara ya Maji, kuona kwamba pendekezo hili la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi kama linaweza likafanyiwa kazi sisi tutakuwa hatuna kipingamizi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kivuko hiki kipya kilinunuliwa mwaka 2007 na hakijafanya kazi kwa muda mrefu na wakati wa masika ni tatizo kwa sababu kinashindwa kupita kwenye maji.

Wakati hakuna maji mengi ni ukame ni tatizo. Je, Serikali ilifanya tathimini gani kabla ya kununua kivuko hiki pengine hela iliyonunulia kivuko hiki ingeweza kutumika kwa ajili ya kujenga barabara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBUNI:** Mheshimiwa Spika, pengine Mheshimiwa Mbunge, hajanisikiliza sawasawa wakati nilipokuwa najibu swali la msingi. Wakati wa kampeni za mwaka 2005 viongozi au wananchi wa katika eneo hili kilio chao kikubwa ilikuwa ni kivuko, kwa sababu kivuko kilichokuwepo kilikuwa hakifanyi kazi ipasavyo cha

tani tano lakini kutokana na kusikia kilio cha wananchi utafiti ukafanyika na fedha zilipopatikana ndiyo kivuko hiki kikanuliwa.

Kwa hiyo, isingekuwa busara kupata fedha hizi kwa ajili ya kujengea kivuko ukakipeleka kwenye barabara ili wananchi waendelee kuteseka na tatizo lile.

Kimsingi utafiti ulifanyika isipokuwa sasa hivi wakati mwingine maji haya yanakuwa yanapata misukosuko ya kupungua na kadhalika wakati mwingine ni katika matumizi tu ya wanadamu ya uharibifu wa mazingira ndiyo haya yanatokea na ndiyo maana hapa nimetoa mwito kwamba wananchi wanaishi katika eneo lile tushirikiane nao kwa kutunza mazingira ili maji yaendelee kuwa ya uhakika kivuko hiki kiendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hiyo hiyo. Niseme tu muda wa maswali kwa sasa ni saa nne kamili lakini kwa sababu tulianza na kubadili Kanuni tuna dakika kadhaa ambazo tumepunguza. Kwa hiyo, tutazifidia kwa kumaliza haya mawili swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Alyoce Kimaro wa Vunjo.

Na. 23

**Ununuzi wa Magari ya Serikali**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

(a) Je, ni magari mangapi yamenunuliwa na Serikali kwa matumizi ya watumishi wake kuanzia mwaka 200-2008 na kwa gharama gani?

(b) Je, njia ipi ni bora ya ununzi wa magari ya Serikali kati ya wizara husika kuagiza mija toka viwandani au kutukia njia ya tenda?

(c) Je, Serikali imeokoa fedha kiasi gani kutokana na agizo la Rais la kusimamisha ununnuzi wa magari ya kifahari ya Serikali (mashangingi).

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aliyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Kabla ya utaratibu huu mpya wa kununua magari ya Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, Taasis zote za Serikali zikiwemo Wizara. Idara, Wakala na Halmashauri za Serikali za Mitaa kila moja zilikuwa zikijinunulia magari kulingana na bajeti yao baada ya kupata *specifications* kutoka Wizara ya Miundombinu.

Mwezi julai 2007, Serikali iliagiza magari yote ya Serikali yanunuliwe kwa pamoja kupitia Wizara ya Miundombinu kwa lengo la kupata ubora na unafuu wa bei. Wizara wakati wa kutekeleza maagizo hayo imekuwa ikifuata taratibu za ununuzi chini ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za Ununuzi za mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo lenye sehemu (a) , (b) , na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2000 hadi mwaka 2008 Serikali imenunua jumla ya magari 4,379 kwa matumizi ya Serikali kwa gharama ya shilingi bilioni 103.51.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za Ununuzi wa Umma za mwaka 2005 ambazo zinaelekea ushindani katika ununuzi wa umma, imekuwa ikinunua magari yake kwa makampuni ya magari yanayoshinda zabuni hizo. Makampuni haya ni mawakala wa kampuni za viwanda vya kutengeneza magari ambavyo vyote viko nje ya nchi.

Mawakala na Viwanda hivi wamejiwekea utaratibu kuwa mawakala hao katika nchi husika ndiyo wanakuwa waagizaji wa magari katika viwanda vyao; na hata Wizara yangu ilipofanya mawasiliano ya moja kwa moja na Viwanda vya *TOYOTA* na *NISSAN* kwa nia ya kuagiza magari toka viwanda hivyo bila kupitia kwa mawakala wao hapa nchini, viwanda hivyo vilielekeza tuagize kupitia kwa Mawakala wao. Kwa hiyo viwanda hivyo haviingii mikataba ya uagizaji wa magari moja kwa moja toka viwandani.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa magari kwa pamoja (*bullk purchase)* una faida kwa Serikali kuliko kununua magari kila Tasasisi peke yake au kwa reja reja kwa kuwa, kwa kununua magari mengi kwa pamoja kuna nafuu ya kupunguziwa gharama.

Kwa mfano, mkataba ambao Serikali ilingia na kampuni ya *Toyota (Tanzania)* mwaka wa fedha 2007/2008 wa kununua magari kwa pamoja (*bulk purchase)* wa shilingi bilioni 53, Serikali ilikuwa na salio au punguzo la shilingi bilioni 5.2 kama ingenunua magari yote kwenye mkataba huu. Hadi sasa Serikali imenunua magari yenye thamani ya shilingi bilioni 47.4 na kupata salio au punguzo la shililngi bilioni 4.17.

(c)Mheshimiwa Spika, Agizo la Mheshimiwa Rais la kusimamisha ununuzi wa magari alilitoa katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi tarehe 31 januari, 2009 agizo ambalo lililenga katika kuokoa fedha za matumizi ya Serikali na kuzielekeza katika shughuli nyingine muhimu za kitaifa, hususani kilimo. Hata hivyo, kwa magari ambayo tayari yalikuwa yamelipiwa fedha kwa Wazabuni hatukuweza kuzirudisha. Kufuatia agizo hilo la Mheshimiwa Rais, Wizara yangu ilisitisha ununuzi wa mashangingi 41 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.3 ambayo *order* yake ilikuwa haijapelekwa kwa Wazabuni.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu ya Serikali, lengo kuu la swali langu, lilikuwa nikuitaka Serikali ipunguze matumizi makubwa ya kuagiza magari ya kifahari. Sasa maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Umoja wa mataifa unatumia utaratibu wa kuagiza moja kwa moja magari yake yote kutoka viwandani. Sasa, kama viwanda vya *NISSAN* na *TOYOTA*, wanakata Serikali kununua moja kwa moja kwa bei nafuu, kwanini Serikaliisiachane nao na kununa kutoka kwenye viwanda vingine kama *LANDROVER*, *HYUNDAI*, *BENZ* bila kutumia tenda kwa kutumia mikataba maalum, kwasababu Serikali inaagiza magari mengi?

(b) Kwa nini magari ya Serikali, na ya mashirika ya Umma yasinunuliwe aina kama tatu ili kurahisisha pia upatikanaji wa vipuri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, mfano nilioutoa kwa hivi viwanda viwili ambavyo havina utaratibu wa kununua magari moja kwa moja, ulijielekeza zaidi kwa kuzingatia kwamba hivi sasa magari mengi tunayoyatumia, yanatoka katika viwanda hivi viwili. Lakini sasa pendekezo hili la kwamba pengine tuangalie uwezekano wa kupata katika viwanda vingine, ni wazo zuri , lakini izingatiwe tu kwamba sas hivi mazoea yetu na magari ambayo tunaona kwamba yana himili barabara zetu hapa nchini na kufanya kazi kwa hufanisi ni katika kampuni hizo mbili nilizo zitaja.

Lakini niseme tu Mheshimiwa Spika, kwamba kusudio lake la kuuliza swali hilo kwamba tulitaka kwamba Serikali izingatie swala la kupunguza garama ya matumiza ya magari, ndio hazma ya Serikali kusema ukweli, na hata haya yote niliyo yaeleza hapa pamoja na maagizo ya Rais, hazma yake na mlengo wake ni huwo huwo wa kupunguza garama ya matumizi ya magari.

Nilisema hapa Bungeni kipindi fulani kwamba hivi sasa inaanda waraka, wakuangalia mpangilio wa matumizi ya magari kufuatana na viwango mbalimbali vya watimishi ambavyo nadhani kwamba ukisha kuwa umekamilika, swala hili ambalo Mheshimiwa analipendekeza hapa, Serikali itakuwa imeshalitimiza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA**: Mheshimiwa Spika, na mimi naomba niulize swali moja dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mwaka jana nikichangia kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Spika, niliiomba Serikali kutengeneza sera ya magari (*car policy)*. Sasa hivi kwenye Serikali, kama alivyosema Mheshimiwa Kimaro, kila Wizara ina kila aina ya magari, kama ni Toyota kuna kutoka Toyota kubwa mpaka chini, kama Nissan ni hivyo hivyo, kuna Wizara nyingine zinatumia Toyota Lexus, *a very luxorious car*, sasa Serikali ya Zambia ina sera ya magari inasema kwamba kwenye Wizara tutatumia gari ya *Prado and Double Cibin*, Serikali ya Rwanda nayo ina sera ya namna hiyo. Je ni lini Wizara yetu itatengeneza sera ya magari?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwambalaswa kama ifuatavyo:-

Tangu mwaka jana katika kufuatilia utaratibu huu wa kudhibiti matumizi ya magari ndani ya Serikali, moja ya vitu ambavyo tunavifanya ni kutathmini aina na madaraja na magari ambayo yanaweza kutumiwa kwa ngazi mbalimbali za watumishi Serikalini, na kuainisha aina chache za magari ambazo zitaweza kutufaa nchi nzima. Hilo ndilo zoezi tunaendelea nalo hivi sasa. Tunatarajia hivi karibuni tutakuwa na maamuzi kuhusu hilo, na swali ambalo Mheshimiwa Mwambalaswa amelizungumzia, ni jambo ambalo tunalipokea na baada ya zoezi hili ya kuainisha ni jambo la pili tutakalolifanyia kazi ni sera ya magari.

**MHE GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa kununua magari kupitia Wizara moja ya Miundombinu, ulikuwa nia nzuri lakini haukufanikiwa vizuri kwa sababu takwimu pamoja na kwamba Naibu Waziri amezisoma hapo, lakini yapo malalamiko kwenye hasa Halmashauri kwamba wamenunua magari kwa bei kubwa. Lakini pia ucheleweshaji umekuwa ni mkubwa mno wa kupata magari hayo. Lakini na kwa kuwa utaratibu huu ulikuwa unakiuka Sheria ya manunuzi ya 2004 na Kanuni zake za

mwaka 2005, kwasababu tu Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu ni *Accounting Officer* kama alivyo Mkurugenzi. Je Serikali, haioni kuna haja kama yenyewe Serikali kuu itaona kwamba kuna haja ya kununua kupitia Wizara ya Miundombinu wafanye hivyo, lakini Halmashauri waziache wanunue gari zao kwa utaratibu wao wenyewe?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunioa nafasi kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa George B. Simbachawene, kama ifuatavyo:

Tangu utaratibu huu umeanza, ni kweli kwamba tumepata malalamiko kadhaa, ya Wizara mbalimbali na Halmashauri na baadhi ya malalamiko haya yamenifikia ofisini kwangu kama waziri. Ni wahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba mengi katika yale matatizo, ambayo yamezungumziwa Halmashauri zimecheleweshewa kupata magari ambayo wameyahitaji, mengi yalikuwa ni matatizo ya mawasiliano. Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba tuliweza kuyatatua na wala hayakuwa hivyo kama ambavyo ilikuwa imesemwa. Tumejaribu kuboresha sana ndani ya Wizara mawasiliano ili tatizo hili la kwamba nani amelipa nini na wengine magari yao kuwepo, tayari yamefika pale hawajaweza kuyachukua kwasababu kukosekana kwa mawasiliano, liwe limeondoka, hatuna tatizo hilo ili tuboreshe utaratibu huu. Kuhusu Kanuni na Sheria ya Manunuzi, manunuzi haya yanafanywa kufuatana na Sheria Namba 21 ya Manunuzi ya Umma, hakuna ununuzi ambao unafanywa nje ya hapo.

Kwa hiyo, yameshindanishwa mashirika au wakala na aliyeshinda ni *Toyota* na kama *report* inavyoonyesha ni kwamba tumeweza ku-*save billion 4.17* mpaka hivi sasa. Sawa sawa na magari makubwa yenye uwezo mkubwa inayokaribia magari 40 na hakuna uwezekano wa kununua magari yale kwa bei ya chini ya hizi zinapatikana kwa sababu huu ni mpango maalum unahusisha magari mengi na Halmashauri hazinunui magari kwa mamia kama ambavyo yananunuliwa kwa pamoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokua anajibu ametuambia kwamba kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais la kusimamisha magari ya kifahari Serikali imeweza ku-*save* 5.3. Na kwa kuwa TEMASA ilianzishwa kwa ajili ya kufanyia matengenezo magari ya Serikali. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuiwezesha na kuimarisha TEMESA ili magari yote ya Serikali yaende kufanyiwa service kule badala ya kufanyia kwenye *garage* za watu binafsi?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Miundimbinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy F. Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa najibu swali la msingi katika kile kipengele cha (c), ni sawa kabisa nilisema kwamba, ile *order* ambayo tulikuwa tumeitoa lakini ilikuwa haijalipiwa, ndio tumeisitisha na ndio maana ilibakizwa zile fedha ambazo nilizitaja katika jibu la msingi na ambalo amelisema hapa Mheshimiwa Mbunge.

Kuhusu swala la magari ya serikali kwenda kutengenezwa TAMESA, kusema kweli hiyo ingekuwa vizuri kwasababu TAMESA inatakiwa itengeneze magari ya Serikali, lakini Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba katika utaratibu wa sasa wa shughuli kwenda huria, kazi za kuendesha shughuli za kibiashara zinakwenda kwa ushindani.

Kwa hiyo, nikubaliane naye tu kwamba sisi kama Serikali ambao tunasimamia ule wakala wa TAMESA tuna wajibu wa kuisimamia TAMESA na kuihimarisha ili iweze ikafanya kazi vizuri ili iingie katika ushindani na asasi zingine zinazofanya kazi hiyo ili waweze wakaweka mvuto zaidi kutengeneza magari ya Serikali. Kwa hiyo nikubaliane naye tu kwamba wajibu wetu wa kuiimarisha TAMESA tutaendelea kufanya hivyo. Lakini kwa sababu ya mazingira ya sasa baadhi ya magari mengine kwenda kufanya matengenezo katika sehemu zingine unaruhusiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali la mwisho kwa siku ya leo, linaelekezwa Wizara ya Fedha na Uchumi, linaulizwa na Mheshimiwa Fatuma Mussa Magimbi, Mbunge wa chakechake.

Na. 24.

**Serikali kuondoa kodi ya *Palm Oil* kutoka nje**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikihamasisha Watanzania kuzalisha mbegu za mafuta ya alizeti *(saf-flower),* katam *(sun flower),* ufuta *(sim sim)*; na kwa kuwa, wakulima walianza kufaidika sana kwa mazao hayo lakini hivi karibuni Serikali imeondoa kodi ya mafuta ya *Palm Oil* kutoka nje.

Je Serikali haioni kwamba, kuondolewa kwa kodi hiyo kunawadhoofisha wakulima hao wa mazao hayo ya mafuta hapa nchini?

**NAIBU WA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Jimbo la Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano ya kuwianisha ushuru wa forodha baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tulikubaliana kuwa mafuta ghafi ya mawese yasitozwe ushuru wa forodha. Sababu kubwa ya uamuzi huu ni kwamba, uzalishaji wa mbegu za kutoa mafuta ya kula katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa sasa, haukidhi mahitaji ya uzalishaji wa mafuta ya kula. Kwa msingi huu tulikubaliana kwamba, mafuta ghafi ya mawese yatakayokuwa yanaagizwa na wazalishai wa mafuta yatozwe ushuru wa asilimia sifuri (0%). Tulipoanza kutekeleza itifaki ya Umoja wa Forodha ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwezi Januari, 2005 tuliwajibika kutumia ushuru wa pamoja *(EAC Common External Tariff)* ambapo mafuta ghafi ya mawese yalitozwa ushuru wa asilimia sifuri (0%).

Mheshimiwa Spika, baada ya mwaka mmoja wa utekelezaji wa itifaki ya Umoja wa Forodha, Tanzania iliwasilisha mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuweka ushuru wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya mawese kutoka nje. Hatua hii ilitokana na maombi ya wadau wa sekta hii kuwa, wangeweza kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mawese na mbegu nyingine za mafuta ndani ya nchi, na hivyo kuviwezesha viwanda kupata malighafi ya kutosha kutoka katika soko la ndani ya nchi. Aidha, ilitarajiwa

kuwa hatua ya kuweka ushuru wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya mawese kutoka nje ingeweza kusaidia kuchochea kukua kwa uchumi wa nchi na kuongeza kipato cha wakulima.

Mheshimiwa Spika, tokea mwaka 2006/2007 hadi mweaka 2008/2009, Serikali imeendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia Kumi (10%) baadala ya asilimia Sifuri (0%), kiwango ambacho kinatozwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Baada ya Tanzania kuweka tena ushuru wa asilimia Kumi (10%) kwenye mafuta ghafi ya mawese yanayoagizwa nje ya nchi, kuna mambo yalijitokeza na kuonekana kuathiri uzalishaji, walaji wa mafuta na wananchi kwa ujumla kama ifuatavyo:-

. Kupanda kwa gharama za kuzalisha mafuta ya kula;
. Kushindwa kunufaika na soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki;

. Tishio la kupanda kwa bei ya mafuta ya kula; na

. Tishio la kufungwa kwa viwanda vya mafuta hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeyatafakari mapungufu niliyoyataja, na inatarajiwa katika hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010 itatoa majibu kuhusiana na suala hili.

**MHE DR. WILLBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa swala la kilimo cha alizeti, katamu ni swala la kulinda pia wakulima wetu. Lakini pia viwanda vyetu ni swala la kulinda ajira zetu. Pamoja na kuangalia maslahi ya Afrika Mashariki, na pamoja na viwanda vyetu vingine ambavyo pia vimeangalia hali kama hiyo. Kwa mfano *General Tyre* ambayo sasa imefungwa.

Je ni nini sera yetu pale ambapo viwanda vyetu vya nadani vinapo athirika kutokana na sera hizi za jumla ni hatua gani Serikali inachukua kuokoa viwanda vyetu vya ndani?

**NAIBU WA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI(MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa fedha na uchumi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Slaa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba ni jukumu la Serikali kulinda viwanda vyetu, ni kweli kwamba kulinda ajira za wana nchi wetu na kuzalisha ajira nyingine, lakini vilevile ni jukumu na ni haki na ni sawa kwamba pale ambapo nchi inakuwa imesha saini itifaki kama tunavyozungumzia itifaki ya nchi za Africa Mashariki. Vilevile kabla hatujachukua hatua zozote. Sio tu tuzingatie yale yalioko kwenye ile itifaki lakini vilevile kuingia kwenye mashauriano na wenzetu. Kwa hiyo katika kuli tafakari hili, kuna mambo mengi ambayo Serikali inapitia lakini hatimaye tunafikia mahali pazuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, maswali yamekwisha na muda umepita kabisa. Sasa ni matangazo. Kwanza wageni na naanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kama ifuatavyo:-

Kwanza ni mkewe, ambaye hapa ameandikwa tu, Mama Mkulo. Bahati mbaya hayupo. Sijui wengine wa familia Mama Astrida Peter, nadhani hawa familia watakuja jioni.

Basi, naomba Waheshimiwa Wabunge tutambue uwepo wa viongozi wa Wizara ya fedha na uchumi na Taasisi zinazohusiana kama ifuatavyo:-

Ndugu Ramadhani Kija, Katibu Mkuu wa Wizara, karibu sana. Ndugu Benal Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)* Bwana Slaa Mkila, Naibu Gavana wa Benki Kuu *(BoT),* naye hayupo
Bibi Marcelina Chijoriga, Mwenyekiti wa *TRA*, hayupo, ahsante sana. Mama muhimu namna hii alitarajiwa kukaa kwenye *Speakers Gallery* sio kumweka mwenyekiti wa *TRA* tena mwanamke mnamweka huku, *Sergeant at arms,* chukua hatua.

Ndugu Harry Kitilia, Kamishna Mkuu wa *TRA* haya sasa, naomba *seargent* ubadili sasa hivi. Haiwezekani mwenyekiti akae alafu mtendaji mkuu akae uapande huu. Ndugu John Haule, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi, yule pale, karibu sana. Ndugu Laston Msongole, Naibu Katibu Mkuu mwingine na Dr Philip Mpango, Naibu Katibu Mkuu. Huyu mpango sio kwamba anashughulikia mipango? Karibuni sana tunashukuru kuwepo kwenu hapa.

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, huyu ni upande wa Upinzani, ana mgeni wake ambaye ni Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti Taifa chama cha *CUF*. Karibu sana *Professor*, tunafurahi mara kwa mara kuwepo kwenye *Budget Session* unakuwa ukija na kwasababu ya taaluma yako nadhani inasaidia. Mgeni wa Mheshimiwa William Ngeleja ni Mheshimiwa Clement Mabina, mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa mwanza, karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Msoma Mjini, ambaye ni wanafunzi wanaosoma *Dodoma University (UDOM)* wasimame, Athumani Koshuma, Zuberi Kiule na Japhet Magesa, wale pale. Karibuni sana,nawatakia mema katika masomo. Wageni wa Ephreimu Madege, ambao ni wafuataao:-

Ndugu Malimi Joram, Rais Mstaafu wa Serikali ya Wanafunzi *UDOM*, yule pale na mkewe labda, Mama Joram, ahsante sana, karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ni Mohamed Iddi Issa, mwenyekiti wa CCM tawi la Bonga Mjini, kuna mji unaitwa Bonga Mjini? *Anyway*, yule pale, Ahsante Sana mwenyekiti.Wageni sita wa Mheshimiwa John M. Cheyo, ambao ni wnafunzi wa *UDOM* kutoka jimbo la Bariadi Mashariki, wale pale pale, karibuni sana tunawatakia masomo mema.

Pia wapo Wawakilishi 51 wa Chama cha CHADEMA, kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na viongozi wao, ambao ni Theodory Mango, wenyekiti yule pale. Ndugu Hamad Abdalah, Kaimu Katibu na Ndugu Nicholas Ngowi au Bwana, Kaimu katibu mwenyezi, naomba basi wale vijana 51 wanachama wa CHADEMA wasimame, ahsante sana. Karibuni sana kwenye ukumbi huu, tunawatakia mema katika masomo yenu.

Waheshimiwa Wabunge nasikitika kutangaza, kifo cha mama yake mzazi wa Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, kilichotokea jana huko Jijini Dar es Salaam, mazishi yatafanyika leo na Katibu amekwisha fanya utaratibu unao stahili kumwezesha Mheshimiwa Mbunge kushiriki kikamilifu katika kumsindikiza Marehemu mama yake mzazi, tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke pema peponi roho ya marehemu. Amina!

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mukulo, ameniomba niwatangazie waheshimiwa Wabunge kuwa kitabu kile cha Hali ya Uchumi ya mwaka 2008 kitaonyeshwa pia kwa njia ya video, kwenye viwanja vya Bunge pale eneo letu la maonyesho pale na pia hatujui ni muda gani lakini, hali ya uchumi kwa mwaka 2008 kitakuwa ni kipindi

maalum kitakachorushwa kwenye Television ya Taifa *TBC1*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaweza kupata fursa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa ofisi imetangaza kwamba Uchaguzi wa Wawakilishi kwenye tume ya huduma za Bunge utafanyika kesho tarehe 12 juni. Lakini taratibu ndani ya vyama vya siasa, inaelekea zitachukua muda. Kwa hiyo uchaguzi huu umeahirishwa hadi mtakapo tangaziwa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa matangazo. Oh! nimepewa sasa hivi kumbe, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tunaye hapa. Tafadhali simama, (*Makofi)*

Ahsante sana Bwana Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Basi Katibu, kwa hatua inayofuata tuendelee.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, hoja za Serikali Waziri wa Fedha na Uchumi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2008 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2009/2010

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili kuweza kupokea na kujadili taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Taifa katika kipindi cha mwaka 2008 na malengo katika kipindi cha muda wa kati 2009/2010 hadi 2011/2012. Pamoja na hotuba hii nawasilisha kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka wa 2008 na kitabu cha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa taarifa yake ya hali ya Uchumi ambayo aliitoa kwa Wazee wa Dodoma pamoja na Wabunge, jana jioni katika Ukumbi wa Kilimani. Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kutupatia ushauri na maelekezo wakati wa kujadili muhtasari wa taarifa hii. Mchango wa kamati hii sikuzote umekuwa na umuhimu wa pekee katika kuboresha taarifa ya hali ya uchumi na mapendekezo ya hali ya bajeti inayowasilishwa katika Bunge lako tukufu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita tangu bajeti ya mwaka jana. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Charles Mwera, Mbunge wa Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Lackson Mwanjale, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Lalensia Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kwa kushinda chaguzi ndogo zilizofanyika katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na familia za Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki dunia katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Hayati Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Hayati

Richard Nyaulawa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Faustine Kabuzi Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Busanda na Hayati Phares Kabuye, ambaye alifariki kabla ya shauri la pingamizi la kutengua Ubunge wake wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kukamilika. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahala pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kutoa muhatasari wa mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo kwa mwaka 2008 ikiwa ni mapitio ya mwaka wa nne wa utekelezaji wa makakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini Tanzania, yaani *MKUKUTA.* Kwa kipindi cha mwaka 2008/2009 bajeti iliendelea kujikita zaidi katika kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii yaliyolenga katika kukuza na kutengemaza uchumi kwa kutekekeleza sera, mipango, programu na mikakati mbalimbali ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu. Aidha ikumbukwe kwamba taarifa hii ni ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2008 na sehemu chache zimegusia robo ya kwanza ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi Jumla Katika Kipindi cha Mwaka 2008. Mwaka 2008 ulikuwa ni mwaka ambao dunia ilikumbwa na matatizo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka huo masoko ya fedha na mitaji yalikumbwa na misukosuko hasa katika nchi zilizoendelea hususan marekani na nchi za ulaya. Aidha tulishuhudia kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kufikia kiwango cha juu zaidi ambacho hakijawahi kutokea na bei za chakula kuwa za juu katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa. Pamoja na kuanguka kwa uchumi wa dunia kulikosababishwa na msukosuko katika sekta ya fedha, pato halisi la Taifa lilikuwa kwa 7.4% mwaka 2008 ikilinganishwa na 7.1% mwaka 2007. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa viwango vya ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo, uvuvi na huduma. Ukuaji wa viwango vya juu ulijionesha katika shughuli ndogo za kiuchumi za mawasiliano (asilimia 20.5); fedha (asilimia 11.9); na ujenzi (asilimia 10.5). Kwa ujumla, kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi kilipungua. Mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma umeendelea kuongezeka katika mwaka 2008 ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Pato la Taifa kutoka shilingi bilioni 20,948.4 mwaka 2007 hadi shilingi bilioni 24,781.6 mwaka 2008 na idadi ya watu Tanzania Bara iliyokadiriwa kuwa watu milioni 39.5, Pato la Wastani la kila Mtanzania liliongezeka hadi shilingi 628,259 mwaka 2008 ikilinganishwa na shilingi 548,388 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.8.

Pato hili la wastani ni sawa na dola za Kimarekani 525.1. Kasi ya Upandaji Bei. Wastani wa kasi ya upandaji bei kwa mwaka 2008 ulikuwa asilimia 10.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2007. Kiwango cha chini cha kasi ya upandaji bei katika mwaka 2008 kilikuwa mwezi Januari ambapo kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 8.6 na kiwango cha juu kilikuwa asilimia 13.5 kilichojitokeza katika mwezi wa Desemba 2008.

Mheshimiwa Spika, lengo tulililoliweka kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei lilikuwa asilimia 5.0 hadi kufikia mwezi Juni, 2008. Lengo hili halikufikiwa kutokana na kuongezeka kwa gharama za nishati, hususan ya umeme, kupanda kwa bei ya mafuta pamoja na bei ya chakula. Hadi Aprili 2009, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 12.0. Kutokana na hali hiyo, lengo la mfumuko wa bei ambalo awali lilikadiriwa liwe chini ya asilimia 7.5 ifikapo Juni 2009 sasa tunatarajia litafikia asilimia 11.0. Mwezi Mei, 2009, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 11.3.

Mheshimiwa Spika, Ukuzaji rasilimali. Katika mwaka 2008, ukuzaji rasilimali uliongezeka kufikia shilingi bilioni 7,381.3 kutoka shilingi bilioni 6,209.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Kuongezeka kwa ukuzaji rasilimali kulitokana hasa na kuongezeka kwa uwekezaji katika ujenzi wa majengo; uagizaji wa vifaa vya uwekezaji mitaji; na kuongezeka kwa shughuli nyinginezo za ukuzaji rasilimali zikiwemo uendelezaji ardhi, barabara na madaraja. Uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 29.7 ikilinganishwa na asilimia 29.6 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Ujazi wa Fedha na Karadha. Katika mwaka ulioishia Disemba 2008, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)1 uliongezeka kwa asilimia 29.7ikilinganishwa na asilimia 27.0 Disemba 2007. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 24.0 Desemba 2008, ikilinganishwa na asilimia 21.4 Desemba 2007. Ongezeko la M2 lilichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwenda sekta binafsi na kuongezeka kwa amana za hundi na za muda maalum.

Mheshimiwa Spika, mikopo iliyoelekezwa katika sekta binafsi iliongezeka na kufikia shillingi bilioni 4,376.4 katika mwaka ulioishia Desemba 2008 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,976.3 zilizotolewa Desemba mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilima 47.0. Ukuaji huu wa mikopo unatokana na Serikali kuendelea kupunguza mikopo yake kutoka vyombo vya fedha vya ndani, kuongezeka kwa uaminifu kwa wakopaji, kuongezeka kwa dhamana ya mikopo *(credit guarantee schemes)*, na kuongezeka kwa mikopo kwa makampuni. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika sekta za: biashara asilimia 16.1; uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 13.1; uchukuzi na mawasiliano asilimia 8.7; kilimo asilimia 8.3; na mikopo binafsi asilimia 19.6.

Mheshimiwa Spika, wastani wa riba zilizotozwa na benki mbalimbali za biashara umeendelea kuwa na pengo kubwa kati ya riba za amana na zile za mikopo. Wastani wa riba za mikopo katika benki za biashara uliongezeka kutoka asilimia 15.25 mwezi Desemba 2007 hadi asilimia 16.05 mwezi Desemba 2008. Aidha, riba za amana za akiba ziliongezeka kutoka asilimia 2.65 mwezi Desemba 2007 hadi asilimia 2.68 mwezi Desemba 2008.

Mheshimiwa Spika, Thamani ya Shilingi ya Tanzania. Thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola ya Kimarekani ilikuwa ni shilingi 1,280.30 mwishoni mwa Desemba 2008 ikilinganishwa na shilingi 1,132.09 mwishoni mwa Desemba 2007. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunatokana na mahitaji makubwa ya dola za Kimarekani kwa makampuni yanayoingiza bidhaa nchini pamoja na baadhi ya makampuni kutaka kuhodhi fedha za kigeni kutokana na ubahatishaji wa kupata faida zaidi *(speculation)*. Hata hivyo, wastani wa mwaka wa thamani ya shilingi ya Tanzania ulikuwa shilingi 1,196.3 kwa dola moja mwaka 2008 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,244.1 kwa dola moja mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Akiba ya Fedha za Kigeni. Mwaka 2008, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 3.9 hadi kufikia dola milioni 2,869.7 kutoka dola milioni 2,761.9 mwaka 2007. Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni mwaka 2008 kilikuwa kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi isiyopungua 4.6 ikilinganishwa na miezi 5 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali; Mapato. Katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 3,199.1, sawa na asilimia 20.4 zaidi ya makusanyo ya kipindi kama hicho mwaka 2007/2008. Hata hivyo, kiasi hiki ni asilimia 9.0 chini ya makisio ya shilingi bilioni 3,529.2 kwa kipindi hicho. Upungufu huu unatokana na kupungua kwa makusanyo ya kodi ya mapato, ushuru wa bidhaa na forodha. Tathmini

iliyofanyika hivi karibuni inaonyesha kuwa hadi Juni, 2009 makusanyo ya mapato ya ndani yatakuwa chini ya lengo kwa takribani asilimia 10, sawa na pengo la shilingi bilioni 480.

Mheshimiwa Spika, Matumizi. Katika kipindi kilichoishia Machi , 2009, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 4,657.9 ikiwa ni asilimia 13 chini ya makisio ya matumizi. Kupungua kwa matumizi hayo kunatokana na upungufu wa makusanyo ya mapato katika kipindi hicho. Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010 nitakayowasilisha leo jioni itabainisha kwa kina mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/09 pamoja na makadirio ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa. Hadi kufikia Desemba 2008, deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani milioni 6,329, ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 5,891.9 Desemba 2007. Deni hilo ni sawa na asilimia 32.6 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.8 ya mwaka 2007. Kati ya kiasi hicho, Dola za Kimarekani milioni 4,822.0 ni deni la nje na Dola za Kimarekani milioni 1,507 sawa na shilingi bilioni 1,929.3 ni deni la ndani. Deni la nje limeongezeka kwa asilimia 14.3 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,218.5 mwaka 2007. Ongezeko hilo limetokana na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris, kushuka kwa thamani ya shilingi na mikopo mipya. Deni la ndani kwa kipindi kinachoishia Desemba 2008 liliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 35 sawa na ongezeko la asilimia 1.8 ukilinganisha na kipindi kilichoishia Desemba 2007. Pamoja na kuongezeka kwa deni la Taifa, bado deni hilo linahimilika *(Sustainable)*.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nje. Mwaka 2008, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Kimarekani milioni 3,036.7 ikilinganishwa na dola milioni 2,226.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia zikiwemo pamba, chai, tumbaku, korosho, kahawa, katani, na karafuu iliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 418.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na dola milioni 319.7 mwaka 2007. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilikuwa dola milioni 2,270.6 mwaka 2008, ikilinganishwa na dola milioni 1,704.5 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 28.8. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya bidhaa za viwandani hasa bidhaa za nyuzi za pamba na katani. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kwa asilimia 113.8 kutoka dola za Kimarekani milioni 309.8 mwaka 2007 hadi dola milioni 662.3 mwaka 2008. Aidha, mapato yatokanayo na biashara ya huduma ikijumuisha utalii, usafirishaji na huduma nyingine yaliongezeka hadi dola milioni 2,168.9 kutoka dola milioni 1,875.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 15.6.

Mheshimiwa Spika, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje iliongezeka hadi dola milioni 6,439.9 mwaka 2008 kutoka dola milioni 4,860.6 mwaka 2007. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji kwa shughuli za kiuchumi katika uzalishaji viwandani, mawasiliano, uchukuzi, ujenzi na madini. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati hasa mafuta iliongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hasa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2008. Hata hivyo, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida ulipungua hususan uagizaji wa chakula ambao ulipungua kutoka dola milioni 315.4 mwaka 2007 hadi dola milioni 290.9 mwaka 2008 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula nchini. Malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola milioni 1,598.0 kutoka dola milioni 1,415.4 mwaka 2007, sawa na asilimia 12.9.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Ulaya na Uswisi iliongezeka kwa asilimia 26.1; nchi za Jumuiya ya Afrika

Mashariki asilimia 82.6; nchi za *SADC* asilimia 47.3; na nchi nyingine za Afrika asilimia 56.4. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za China, Japan, India, Hong Kong na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 61.5 na Bara la Amerika kwa asilimia 51.1.

Mwaka 2008, nakisi katika urari wa biashara nje iliongezeka hadi dola milioni 2,333.4 ikilinganishwa na dola milioni 2,041.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Nakisi hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola milioni 108.8 mwaka 2008 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 412.6 mwaka 2007. Ziada hii, kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na misamaha ya madeni iliyotolewa na wahisani katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi Duniani na Ushirikiano wa Kimataifa. Kiwango cha ukuaji wa biashara duniani kiliendelea kushuka kutokana na mahitaji madogo ya bidhaa kwa Nchi Zilizoendelea na hivyo kusababisha kushuka kwa ukuaji wa biashara ya kimataifa. Katika mwaka 2008, Pato la dunia lilikua kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2007. Kupungua kwa Pato la dunia kulitokana hasa na kuendelea kuporomoka kwa uzalishaji katika Nchi Zilizoendelea kiuchumi hususan Marekani kulikosababishwa na kuporomoka kwa soko la fedha na mitaji.

Mheshimiwa Spika, Pato la Nchi Zilizoendelea lilikua kwa asilimia 1.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2007. Kushuka kwa ukuaji wa Pato la Nchi Zilizoendelea kulitokana na kupanda kwa bei za mafuta na kupungua mauzo nje. Kwa upande wa Nchi Zinazoendelea na Nchi za Asia zinazoinukia kiviwanda, wastani wa Pato ulipungua hadi asilimia 6.9 na 8.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.9 na 9.7 mwaka 2007 kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika. Kiwango cha ukuaji wa Pato la Bara la Afrika kilipungua hadi wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2007. Kupanda kwa bei ya mafuta husani kwa nchi zisizozalisha mafuta, ukame kwa baadhi ya maeneo na migogoro ya kisiasa kulisababisha kupungua kwa ukuaji wa uchumi Barani Afrika.

Aidha, Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara lilikua kwa wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda na Kimataifa. Ushirikiano wa Tanzania kimataifa na kikanda uliendelea kuimarika na hivyo kuendelea kulijengea taifa mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Kanda hizo ni pamoja na za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika *(NEPAD)* pamoja na Shirika la Kimataifa la Biashara *(WTO)*.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2008, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea na majadiliano ya kuunda Soko la Pamoja la Jumuiya ambalo linatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2010.

Vile vile, katika jitihada za kuimarisha ushirikiano, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga hadi *Athi River (Kenya)* ulisainiwa mwaka 2008. Aidha, miradi kwa ajili

ya kuimarisha upatikanaji wa umeme kati ya Kenya na Tanzania ilianza katika miji ya Longido na Namanga.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Katika mwaka 2008, Mpango wa kuwa na Eneo Huru la Biashara *(SADC – FTA)* ulizinduliwa katika mji wa Sandston, Afrika ya Kusini na ulianza rasmi Januari 2008. Mpango huu unatoa fursa ya kufanya biashara bila ushuru katika Kanda kwa asilimia 85.

Aidha, Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki, na Kusini mwa Afrika *(COMESA)*; na Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya Mkutano wa pamoja kwa lengo la kuendeleza muungano wa jumuiya hizo. Wakuu wa nchi walikubaliana kuanzisha Eneo Huru la Biashara ambalo litajumuisha Jumuiya zote tatu na hatimaye kuwa na umoja wa forodha. Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika *(NEPAD)*.

Katika mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika uliofanyika Juni 2008, Wakuu wa Nchi na Kamati ya Utekelezaji wa *NEPAD* walikubaliana kuhusu mapitio ya utekelezaji wa *NEPAD* kwa lengo la kuharakisha utengemazi wa *NEPAD* kwenye mfumo wa Jumuiya ya Afrika.

Aidha, iliamuliwa kuwa mchakato na masuala yote ya utengemazi wa *NEPAD* kwenye mfumo wa Jumuiya ya Afrika uwe umekamilika kabla ya kikao cha kawaida cha 20 cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kamati ya Utekelezaji wa *NEPAD*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kimataifa la Biashara. Tanzania iliendelea kushiriki na kuunga mkono majadiliano ya biashara baina ya nchi wanachama wa Shirika la Kimataifa la Biashara. Hata hivyo, majadiliano yalivunjika Julai 2008 baada ya kushindwa kufikiwa muafaka kati ya Nchi Zilizoendelea na Nchi Zinazoendelea juu ya suala la utoaji wa ruzuku ya mazao ya kilimo kwa Nchi Zilizoendelea wakati Nchi Zinazoendelea zinashinikiza kupunguza ruzuku katika mazao. Maendeleo ya Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi na Kijamii. Mawaziri wa maeneo husika wataeleza kwa kina maendeleo katika maeneo yao; hivyo katika hotuba hii, nitaelezea kwa kifupi kuhusu maendeleo ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kilimo, Mifugo, Misitu na Uwindaji. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo, mifugo, misitu na uwindaji kiliongezeka kwa asilimia 4.6 mwaka 2008 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2007/08; kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji na barabara vijijini; jitihada za Serikali za kuwasambazia wakulima pembejeo za kilimo kama mbolea ya ruzuku na zana za kilimo; na kuhimiza ufugaji wa kibiashara. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao kiliongezeka kutoka asilimia 4.5 mwaka 2007 hadi asilimia 5.1 mwaka 2008.

Kwa kuzingatia mabadiliko ya mgawanyo wa mazao na mahitaji yake, utaratibu uliokuwa ukitumika awali wa kugawa mazao katika makundi mawili: ya chakula na biashara kwa sasa hautumiki tena, kwani sehemu kubwa ya mazao ambayo yalikuwa yanajulikana kama ya chakula yaliuzwa hususan katika nchi za jirani. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 2.4 mwaka 2007 hadi asilimia 2.6 mwaka 2008. Sababu zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na: upatikanaji wa malisho ya kutosha; na kuongezeka kwa huduma za ugani katika shughuli za uendelezaji kilimo na mifugo.

Shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.4 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2007. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ada za uwindaji wa kitalii pamoja na ada za vibali vya kukamata wanyamapori hai.

Mheshimiwa Spika, kama nitakavyoeleza baadaye leo jioni katika hotuba ya bajeti, kaulimbiu ya serikali mwaka 2009/10 ni "Kilimo Kwanza" na bajeti itajielekeza zaidi katika kutekeleza hilo. Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na barabara za vijijini, pamoja na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo, na vile vile kupunguza athari za kuanguka kwa uchumi wa dunia katika uchumi wa Tanzania.

Maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kuongeza ubora wa bidhaa za kilimo na upatikanaji wa masoko; kuongeza upatikanaji wa mikopo ya kilimo na yenye gharama nafuu; kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo kama vile mbolea, mbegu bora na zana za kilimo; kuendelea kuboresha upatikanaji wa chakula cha kutosha, kupanua kilimo cha umwagiliaji na kuongeza hifadhi ya Taifa ya chakula; kuimarisha ufanisi na upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima na wafugaji; kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, majosho na machinjio ya mifugo; kuendeleza viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo; kuongeza na kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kuuza nje; kupunguza uvunaji wa misitu usio endelevu na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuweka usimamizi endelevu wa misitu na vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi. Shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 5.0 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2007. Ongezeko hilo lilitokana na udhibiti wa uvuvi haramu; na uboreshwaji wa mazingira ya mazalia ya samaki. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa ulipungua kidogo na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2008 kutoka asilimia 1.3 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, maeneo ya kipaumbele yatakuwa ni:-

Kupitia upya Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997 ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo; kuendelea kukabiliana na uvuvi haramu; na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kuhifadhi samaki.

Mheshimiwa Spika, Viwanda na Ujenzi. Kiwango cha ukuaji wa uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 9.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2007.

Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa viwandani hususan bidhaa za chakula na maziwa, kemikali na uchapishaji; na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zilizouzwa nje. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.8 mwaka 2008, sawa na ilivyokuwa miaka miwili iliyotangulia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha muda wa kati, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika uzalishaji viwandani ni pamoja na kuendeleza viwanda vya msingi, kuongeza thamani ya bidhaa na kupunguza uuzaji wa mazao ghafi nje. Shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa asilimia 10.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2007.

Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na upanuzi wa miundombinu ya maji. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.7 mwaka 2008 ukilinganisha na asilimia 7.8 mwaka 2007.

Malengo ya mwaka 2009/2010 ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa barabara kama ilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilikuwa asilimia 5.4 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2007. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa ufuaji wa umeme wa gesi na makaa ya mawe na kumalizika kwa muda wa Mikataba ya Dowans, APR na Aggreko. Shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi zilichangia asilimia 1.7 katika Pato la Taifa mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha muda wa kati, juhudi zitaelekezwa katika ufuaji umeme, usafirishaji na usambazaji na kuongeza upatikanaji wa nishati ya kisasa vijijini. Aidha, serikali itaendelea na mchakato wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta na upanuzi wa miundombinu ya gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika, ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe ulishuka kutoka asilimia 10.7 mwaka 2007 hadi asilimia 2.5 mwaka 2008. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uzalishaji katika migodi mikubwa kulikosababishwa na mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa sehemu ya miundombinu ya uchimbaji katika mgodi wa dhahabu wa Geita, ambao ndiyo mkubwa kuliko yote nchini, kuliathiri uzalishaji wa dhahabu kwa kiasi kikubwa. Aidha, mabadiliko ya umiliki wa mgodi wa almasi wa Williamson, ambapo kasi ya uzalishaji katika kipindi cha mpito kwa wamiliki wapya ilipungua na vile vile walisitisha uuzaji wa almasi nje. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2007 hadi asilimia 3.4 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuifanyia marekebisho Sera ya Madini ili kuiwezesha sekta ya madini kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Maboresho katika sekta ya madini yatalenga katika kuongeza ushirikishwaji wa wananchi, kuboresha mfumo wa sheria na kodi na pia kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shughuli za utoaji huduma za kiuchumi zinajumuisha biashara na matengenezo; uchukuzi; mawasiliano; hoteli na migahawa; utawala; elimu; afya; huduma za fedha na bima; na upangishaji wa majengo. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikua kwa asilimia 8.5 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2007. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.7 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 43.3 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, shughuli za mawasiliano katika mwaka 2008 zilikua kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko shughuli nyingine zote za huduma za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji kwa shughuli hizi kilikuwa asilimia 20.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 20.1 mwaka 2007. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliongezeka hadi kufikia asilimia 2.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, shughuli za huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.9 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara na kuongezeka kwa abiria katika safari za anga za kimataifa. Mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa, umeendelea kuwa asilimia 4.2 mwaka 2008, sawa na ilivyokuwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, kipaumbele katika shughuli za kiuchumi za mawasiliano na uchukuzi, kitawekwa kwenye kuendeleza miundombinu ya usafirishaji, pamoja na kuongeza kasi ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na jamii kwa ujumla katika kuendeleza shughuli hizi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 10.0 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 9.8 mwaka 2007. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa biashara nchini. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 11.6 ya Pato la Taifa mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 11.5 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, shughuli ndogo za hoteli na migahawa (ikijumuisha utalii), zilikua kwa asilimia 4.5 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2007. Ukuaji huo ulitokana na mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Mchango wa shughuli za huduma za hoteli na migahawa katika Pato la Taifa ulishuka kidogo kufikia asilimia 2.6 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2007. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kuboresha Sekta ya Utalii kwa kuhimiza utalii wa ndani; kutangaza vivutio vya utalii wetu nje; na kutafuta masoko hususan nchi za Asia.

Mheshimiwa Spika, shughuli za huduma za kifedha zilikua kwa asilimia 11.9 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mikopo kwa sekta binafsi; mahitaji ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji; huduma za bima; na huduma za kibiashara. Mchango wa shughuli za huduma za kifedha katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 mwaka 2008 sawa na ilivyokuwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa huduma za upangishaji majengo na huduma za biashara ulikuwa asilimia 7.1 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2007. Mchango wa shughuli za upangishaji majengo na huduma za biashara katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 9.6 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 9.5 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008, shughuli za utawala zilikua kwa asilimia 7.0, ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma. Mchango wa shughuli za utawala katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.2 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji katika shughuli za huduma ya elimu kilikuwa asilimia 6.9 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2007. Ukuaji katika shughuli hizi ulitokana na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Mchango wa shughuli za huduma za elimu katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.3 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha muda wa kati, juhudi zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuboresha usimamizi wa mfumo wa mawasiliano katika Sekta ya Elimu.

(ii) Kuboresha utoaji wa elimu maalum; na

(iii) Kupanua na kuboresha miundombinu kwa ajili ya taasisi za elimu ya juu ili kukidhi mahitaji yatakayotokana na utekelezaji wa MMEM na MMES.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji katika huduma za afya kilikuwa asilimia 9.0 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2007. Aidha, ukuaji huu ulichangiwa na utekelezaji wa programu za chanjo, malaria, kifua kikuu na VVU na UKIMWI. Mchango wa shughuli za huduma za afya katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2009/10, Serikali itaweka mkazo katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Huduma ya Afya ya Msingi;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano; na

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kulingana na makadirio ya kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9 cha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2002, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa milioni 40.7 mwaka 2008. Kati yao; watu milioni 20.7 sawa na asilimia 50.9, walikuwa ni wanawake na watu milioni 20.0 sawa na asilimia 49.1 walikuwa ni wanaume. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na jumla ya watu milioni 39.5 na Tanzania Zanzibar watu milioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa idadi ya watu kulingana na umri ni kama ifuatavyo: Watu wenye umri chini ya miaka 15 ni asilimia 44.4 ya watu wote; watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 ni asilimia 19.8; idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 64 ni asilimia 32.4; na watu wenye umri zaidi ya miaka 65 walikuwa ni asilimia 3.4 ya watu wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008, nguvukazi nchini iliendelea kuwa watu milioni 20.6 kulingana na matokeo ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi *(Integrated Labour Force Survey - ILFS*) wa mwaka 2005/06. Vile vile matokeo hayo yanaonyesha kuwa watu milioni 18.3 walikuwa wana ajira. Kati yao, watu milioni 9.0 walikuwa wanaume na wanawake walikuwa milioni 9.3. Katika mwaka 2008, Serikali ilianzisha Wakala wa Huduma za Ajira ili kusaidia kutoa huduma bora zinazohusu ajira hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha watu wanaotafuta kazi na waajiri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha Utawala Bora, mwaka 2008, Serikali iliendelea kuboresha taratibu za uchaguzi na kuimarisha demokrasia nchini kwa kuanza kuhuisha Sheria ya Uchaguzi Sura ya 343 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Aidha, katika mwaka 2008, Tume ya Uchaguzi ilianza zoezi la kuhakiki daftari la wapiga kura nchini. Lengo ni kurekebisha taarifa za wapiga kura kwa waliohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine,

kuwasajili waliofikisha umri wa kupiga kura na kuwaondoa waliopoteza sifa za kupiga kura na waliofariki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008, Serikali ilianza kufanya utafiti wa kutathmini hali ya rushwa na Utawala Bora nchini *(National Governance and Corruption Survey*) na matokeo ya utafiti huu yatatolewa mwishoni mwa mwezi Juni, 2009. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha shughuli za Mahakama, mwaka 2008, Majaji wapya 15 waliteuliwa; Mahakimu Wakazi na wa Wilaya 95; na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 128 waliajiriwa. Kufuatia kuongezeka kwa watumishi hao, Mahakama ya Rufaa iliweza kusikiliza mashauri 1,189 kati ya 3,043 yaliyokuwepo. Mahakama Kuu ilisikiliza mashauri 4,683 kati ya mashauri 14,152 yaliyokuwepo. Kwa upande wa Mahakama za Mikoa na Wilaya, jumla ya mashauri 30,615 yalipangwa kusikilizwa na kati ya hayo mashauri 17,595 yalisikilizwa. Mahakama ya Biashara ilisikiliza mashauri ya kibiashara 117 yaliyofunguliwa na mashauri 90 yalitolewa maamuzi. Mahakama ya Kazi ilikamilisha mashauri 364 yanayohusu migogoro ya kazi kati ya mashauri 577.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), ulisajili jumla ya vizazi 2,268,272; vifo 117,295; na ndoa 12,295; ikilinganishwa na vizazi 829,384; vifo 118,538 na ndoa 46,320 mwaka 2006/07 kwa mtiririko huo. Aidha, jumla ya watoto 27 wa kuasiliwa waliandikishwa na kupata vyeti.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na uharibifu wa mazingira, Serikali iliendelea kutekeleza sera, mikakati, sheria na kanuni zinazolenga kuwa na utumiaji endelevu wa mazingira kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa shughuli za mazingira katika mwaka 2008, ulikuwa kama ifuatavyo: Wilaya 37 zilivuka lengo la kupanda miti milioni 1.5; Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini kwa kipindi cha mwaka 2007/08 ilikamilika; Mikataba ya Kimataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; na mradi wa usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika ulianza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Janga la UKIMWI limeendelea kuwa ni tishio kwa maendeleo ya Taifa. Athari zake zimeendelea kusambaa kwa familia na jamii. Katika mwaka 2007/08, watu wanaoishi na VVU wenye umri kati ya miaka 15 - 49 walikadiriwa kuwa asilimia 5.7. Kasi ya maambukizi ya UKIMWI inakadiriwa kuwa asilimia 5.8, ambapo maambukizi kwa wanawake ni asilimia 6.6 na wanaume asilimia 4.6. Mwaka 2008, idadi ya watu wanaoishi na VVU na wanaopata tiba ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, iliongezeka hadi watu 193,978 kutoka watu 69,250 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Pili wa Sekta mbalimbali, juu ya VVU na UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2008 - 2012. Mpango huo unalenga katika kuelekeza njia mbalimbali za kudhibiti maambukizi ya UKIMWI. Aidha, mwaka 2008, mkakati wa kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ulipanuliwa hadi katika ngazi za vituo vya msingi vya afya nchini. Mkakati huo unalenga kuwa na watoto wanaozaliwa ambao hawajaambukizwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008, Serikali iliendelea kuweka msisitizo katika kuingiza masuala ya jinsia katika sera za kisekta na zile za jumla. Katika kufanikisha hilo, mafunzo ya uingizaji masuala ya jinsia katika maeneo hayo yalitolewa kwa watendaji mbalimbali wakiwemo Makatibu Wakuu wa Wizara, Waratibu wa Jinsia katika Wizara na Kamati za Jinsia za Kisekta.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu maendeleo ya jinsia kwa kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia uwiano wa kijinsia. Aidha, Serikali imetafsiri Azimio kuhusu Usawa wa Jinsia Afrika (*Solemn Declaration on Gender Equality in Africa*) na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Unyanyasaji wa Wanawake; katika lugha rahisi (*popular version*), kwa lengo la kuwafikishia ujumbe walengwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais jana alieleza kwa upana zaidi juu ya Msukosuko wa uchumi duniani na athari zake kwa uchumi wa Tanzania, lakini mimi pia nitaligusia kidogo suala hili. Chimbuko la msukosuko wa uchumi duniani lilitokana na watu wengi nchini Marekani, kushindwa kurejesha mikopo ya nyumba kufuatia kupanda kwa riba na kusababisha sekta ya fedha kuvurugika. Aidha, hali hii ilisababisha kuporomoka kwa masoko ya fedha na mitaji nchini Marekani na kusambaa katika masoko ya fedha na mitaji ya nchi zilizoendelea na zinazoinukia kiuchumi. Kutokana na msukosuko huu, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), linakisia ukuaji hasi wa asilimia 1.3 kwa uchumi wa dunia kwa mwaka 2009. Hali hii imesababishwa na ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 3.8 kwa nchi zilizoendelea. Aidha, ukuaji wa pato kwa nchi zinazoinukia na zinazoendelea, utashuka kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2008 hadi wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2009. Pato la nchi za Afrika litashuka hadi asilimia 2.0 mwaka 2009 kutoka asilimia 5.9 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishachukua hatua za awali za kupunguza au kukabiliana na athari za msukosuko huu wa uchumi. Kwa kuzingatia chanzo cha msukosuko huu, Benki Kuu imekuwa na utaratibu wa uangalizi na usimamizi wa mabenki kila siku ili kuweza kubaini matatizo yatakayojitokeza na kuchukua hatua za haraka. Aidha, katika kupunguza makali na kuhimili shinikizo la msukosuko hususan kuwalinda wananchi walio kwenye hatari kubwa zaidi, Serikali inalenga katika kutekeleza yafuatayo: Kulinda ajira hasa katika baadhi ya shughuli zitakazokumbwa na matatizo ya ukwasi kutokana na kupungua kwa utashi wa bidhaa na huduma wanazozalisha; kuinusuru nchi kutokana na athari za upungufu wa chakula duniani zilizochochewa na msukosuko pamoja na hali mbaya ya hewa; kulinda programu muhimu za kijamii; na kulinda uwekezaji muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na programu mbalimbali za muda mrefu, kati na muda mfupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ni mpango wa muda mrefu, ambao unalenga kuwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania iwe ni miongoni mwa nchi zenye viwango vya kati vya mapato *(Middle Income Country*) na hali bora ya maisha. Mpango huu unalenga kwamba, Tanzania ya mwaka 2025 iwe na sifa zifuatazo: maisha bora na mazuri; amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi bora; jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na uchumi wenye uwezo wa ushindani na kujiletea ukuaji endelevu kwa maslahi ya watu wote. Tangu Dira hii kuanza kutekelezwa mwaka 2000, Serikali imekuwa ikiandaa mikakati ya muda wa kati ya utekelezaji wa Dira *(Medium Term Plan*) na kila sekta inaagizwa kuandaa mpango mkakati (*Strategic Plan*) wa kufikia malengo ya Dira. Pia kulikuwepo na mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini (*PRS* I), ambao utekelezaji wake ulifanyika kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2000/01 – 2003/04. Utekelezaji wa Dira unaendelea kupitia mipango, mikakati na programu mbalimbali za muda wa kati na muda mfupi ikiwemo:-

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*); na Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya

Tanzania 2020 (*Mini-Tiger Plan* 2020). Baada ya miaka kumi ya utekelezaji wa Dira, Serikali inafanya tathmini ili kujua mafanikio na changamoto zilizojitokeza na mikakati ya kuzikabili. Zoezi hilo linaendelea na taarifa rasmi itawasilishwa serikalini na mshauri mwelekezi mwishoni mwa Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), utekelezaji wa MKUKUTA ambao unalenga kufikia malengo ya Dira 2025 umekuwa na mafanikio katika maeneo yake yote matatu. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, viashiria vinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko katika ukuaji wa Pato la Taifa; ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuimarika kwa miundombinu hasa ya barabara. Ukuaji huu umejidhihirisha katika kupungua kwa umaskini.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kwa Tanzania Bara uliofanyika mwaka 2007, unaonesha kuwa idadi ya Watanzania wasiojitosheleza kwa mahitaji ya msingi, imeshuka kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/01 hadi asilimia 33.4 mwaka 2007 na wasiojitosheleza kwa chakula imepungua kutoka asilimia 18.7 mwaka 2000/01 hadi asilimia 16.5 mwaka 2007. Hata hivyo, Serikali inaona kuwa kasi ya kupungua kwa umaskini hairidhishi; hivyo, hatua zitachukuliwa za kuongeza kasi ya kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/08, mafanikio pia yalipatikana katika sekta za huduma ya jamii. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa uandikishaji wanafunzi katika shule za awali kutoka 795,011 mwaka 2007 hadi 873,981 mwaka 2008; msingi kutoka 8,316,925 mwaka 2007 hadi 8,410,094 mwaka 2008; sekondari kutoka 829,094 mwaka 2007 hadi 1,035,373 mwaka 2008 na vyuo vya elimu ya juu kutoka 60,716 mwaka 2007 hadi 100,394; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule za sekondari; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu waliopatiwa mikopo; kuboreshwa kwa huduma za afya; na upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na kutokuwepo kwa uwiano mzuri kati ya wanafunzi na walimu katika shule; mazingira yasiyoridhisha ya kujifunzia na kufundishia; kutokuwepo kwa uwiano sawa wa kijinsia hasa katika shule za sekondari na elimu ya juu; na kiwango cha juu cha vifo vya mama wajawazito na watoto. Serikali inachukua hatua za kurekebisha hali hii kulingana na uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, katika suala la Utawala Bora na Uwajibikaji, vyombo vinavyohusika na haki za binadamu vimefanya kazi nzuri hadi sasa na vitaendelea kuongezewa uwezo wa kiutendaji. Aidha, Serikali iliendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), jumla ya miradi 2,750 iliibuliwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2008. Kati ya miradi hiyo, miradi 2,210 ilipatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Hadi mwishoni mwa Desemba 2008, jumla ya miradi 5,657 yenye thamani ya shilingi bilioni 126.2 iliibuliwa tangu TASAF Awamu ya Pili ianze.

Kati ya miradi hiyo, miradi 3,700 ilikuwa kwa ajili ya jamii zenye ukosefu wa huduma za kijamii, miradi 1,628 kwa ajili ya makundi maalumu na miradi 349 kwa ajili ya kaya zenye upungufu wa chakula lakini zina watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Awamu ya Pili ya TASAF inatekelezwa katika Halmashauri 133 za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, Serikali ilitayarisha Mpango Maalumu wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini Tiger Plan 2020)*, kwa kuzingatia uzoefu na mafanikio ya nchi za Kusini Mashariki mwa Asia. Uzoefu wa nchi hizi unafaa kwa maendeleo ya Taifa letu kwa kuwa miaka takriban arobaini iliyopita, baadhi ya nchi hizo zilikuwa sawa na Tanzania kimaendeleo na nyingine hata kuwa nyuma, lakini pamoja na hatua nyingine, kwa kuanzisha mipango maalumu iliyobuniwa kuvutia uwekezaji, nchi hizi zimeweza kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mpango huu ni kuanzisha maeneo maalumu ya uwekezaji kwa ajili ya shughuli za viwanda, kilimo, utalii, upandaji miti na TEKNOHAMA. Mojawapo ya maeneo hayo ni ujenzi wa eneo maalumu la uwekezaji la *Benjamini William Mkapa Special Economic Zone* (*BWM-SEZ*) lililoko Mabibo Dar es Salaam, ambao umefikia hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Juni 2009. Taratibu za kupata wawekezaji katika eneo husika zimeshaanza na tayari maombi ishirini yamekwishapokelewa kutoka kwa wawekezaji mbalimbali na yanashughulikiwa kulingana na vigezo vilivyoainishwa na mamlaka husika. Eneo hili litakapokamilika, litakuwa na uwezo wa kutoa ajira mpya zisizopungua 20,000. Aidha, Kampuni za *Oji Paper* na Marubeni za Japan, kwa kushirikiana na Chuo cha Utafiti cha Naliendele, tayari zimeshaanza miradi ya kupanda miti kwenye mashamba ya majaribio katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Lengo ni kuotesha misitu ya mbao kwa ajili ya kutengeneza karatasi ambazo zina soko kubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mafanikio yamepatikana katika utoaji wa mikopo na uanzishwaji wa *SACCOS* na vikundi vidogo vidogo vya kiuchumi vya vijana na wanawake. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia mifuko na programu mbalimbali ikijumuisha Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato; Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi; na Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo (*SELF*).

Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2009, awamu ya kwanza ya Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Benki za NMB na CRDB, ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 42.48, ikiwa ni asilimia 37.0 zaidi ya lengo la shilingi bilioni 31.0. Jumla ya wajasiriamali 65,508 walinufaika na mikopo hiyo kupitia SACCOS 192 na vikundi 86.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, ilizinduliwa mwezi Januari 2008. Katika awamu hii, jumla ya shilingi bilioni 9.9 zilitolewa kwa benki na asasi 12 za fedha ambazo zilikopesha fedha hizo kwa walengwa kwa kuzingatia masharti nafuu ya ukopeshaji yaliyoidhinishwa na Serikali. Pia kiasi cha shilingi milioni 600 zilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili hiyo. Katika awamu hii, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.7 ilitolewa na benki na asasi za fedha zilizoidhinishwa kwa wajasiriamali 22,150 katika wilaya 21 ambazo hazikupata fedha katika awamu ya kwanza na wilaya 46 zilizopata chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi *(Mwananchi Empowerment Fund)*, ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwezeshaji Namba 16 ya Mwaka 2004. Mfuko huo ulizinduliwa Januari, 2008 ukiwa na kianzio cha shilingi milioni 400. Madhumuni ya Mfuko huo ni kudhamini mikopo ya wajasiriamali (Wadogo, Kati na Wakubwa), ambao wanashindwa kupata mikopo kwenye benki za biashara kwa sababu ya kukosa dhamana.

Mheshimiwa Spika, hadi mwishoni mwa Machi 2009, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 1,280 kwa SACCOS 18 za Mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara na

Rukwa, ambapo wajasiriamali 720 walinufaika. Mikopo hiyo ilielekezwa kwenye shughuli za uzalishaji mali hususan kilimo. Aidha, uhamasishaji wa wajasiriamali kujiunga katika *SACCOS* ulifanyika na kufanikiwa kuongeza idadi ya *SACCOS* kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi *SACCOS* 4,780 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo *(SELF)*, ambao ulianzishwa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kupata mitaji hususan walioko vijijini. Hadi Machi 2009, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 19.2 ilikuwa imetolewa kupitia asasi ndogo za fedha zipatazo 206 na walengwa 64,446 walikuwa wamenufaika na mikopo hiyo; kati ya hao asilimia 58 ni wanawake. Kwa wastani, kiwango cha marejesho kutoka kwa asasi ndogo za fedha zilizokopeshwa kilikuwa asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi huo wa *SELF*, mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa watendaji wapatao 1,889 kutoka katika asasi ndogondogo za fedha zikiwemo SACCOS 373 na Mashirika Yasiyo ya Serikali *(NGOs)* 33. Katika idadi hii asasi 85 ziko Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kipindi cha 2009/10 ni pamoja na kubuni mikakati mbalimbali ya utekelezaji wa Sera; kutafuta vyanzo vya fedha na kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali; kuratibu na kutathmini shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuandaa mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi; kutoa mafunzo kwa wajasiriamali; kubuni na kuratibu tafiti mbalimbali zinazolenga kuongeza tija; na kuboresha upatikanaji wa taarifa muhimu za masoko ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia hilo, hatua zinachukuliwa kuboresha mazingira ya kuziwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na utekelezaji wa programu mbalimbali kama vile MKURABITA na MKUMBITA. Hali kadhalika, kukamilika kwa Sera ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi *(Public Private Partinership Policy*), kutasaidia katika kuharakisha maendeleo ya sekta binafsi na kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni mpango ulioanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba 2004, ukilenga kuwapa wananchi nguvu kiuchumi, hasa wale wa kipato cha chini vijijini na mijini, kwa kuwaongezea uwezo wa kumiliki rasilimali na kufanya biashara katika mfumo rasmi wa kisasa, unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni rasmi za kiutawala. Utekelezaji wa MKURABITA umepangwa katika awamu nne na utekelezaji wa awamu ya pili, yaani Maandalizi ya Maboresho, ulikamilika mwaka 2008. Katika hatua hii, maeneo mbalimbali yalipendekezwa kufanyiwa maboresho katika azma ya kufikia malengo ya MKURABITA. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kurasimisha umiliki wa ardhi, kuruhusu matumizi ya ardhi kwa matumizi ya maendeleo kiuchumi na kurasimisha biashara kwa kuondoa vikwazo. Hatua ya tatu ya utekelezaji wa MKURABITA ambayo ni Utekelezaji wa Maboresho imeanza. Lengo kuu katika hatua hii ni kutekeleza hatua za maboresho zilizopendekezwa katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA), Serikali iliweka kipaumbele katika kurekebisha mfumo wa sera, sheria na taratibu katika maeneo ambayo mazingira wezeshaji yanatoa nafasi ya pekee ya kuchangia

maendeleo ya sekta binafsi. Ili kupunguza urasimu wa kufanya biashara nchini, Serikali itatekeleza Sheria ya Uandikishaji wa Shughuli za Biashara (BARA) ya mwaka 2007, ambayo inaanza kwa Halmashauri 24. Uzoefu utakaopatikana utasaidia katika kuelewa faida na changamoto zilizopo ili kupendekeza maboresho au mabadiliko katika Sheria hiyo au kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008, MKUMBITA uliendelea kuchangia kujenga uwezo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika maeneo yanayohusu utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Vijijini ya Mwaka 1999 ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Sheria hiyo kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingine katika eneo hili ambayo Serikali inaendelea kutekeleza ni pamoja na Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Mradi huu unaendelea na maelezo zaidi yatatolewa na Wizara husika wakati wa kuwasilisha hotuba ya Bajeti yake. Mradi mwingine ni wa upimaji wa ardhi ya vijiji 1,500 vilivyobaki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Baraza la Taifa la Biashara, liliendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Aidha, Baraza liliendesha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi jinsi ya kuboresha mazingira ya biashara. Baraza limefungua matawi mikoa yote na tayari Mabaraza ya Wilaya yameanzishwa kwa nia ya kuboresha mazingira ya Biashara katika ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008, Baraza la Taifa la Biashara lilifanya mikutano ifuatayo: Mkutano wa Tano wa Baraza la Taifa la Biashara kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mkutano wa Tatu wa Wawekezaji wa Ndani (*Local Investors' Round Table*); na Mkutano wa Saba wa Wawekezaji wa Nje *(International Investors' Round Table*). Madhumuni ya mikutano hii ni kuhamasisha uwekezaji kutoka nje na ndani kwa kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliongezeka kufikia Dola za Kimarekani milioni 695.5 mwaka 2008, ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 653.4 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Aidha, nchi ya Uingereza iliendelea kuongoza katika nchi zenye miradi mingi ya uwekezaji mwaka 2008 ikiwa na miradi 96; Kenya 72, China 50, India 39, Uholanzi 27, Marekani 24 na Afrika Kusini 20.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, kaulimbiu ya Serikali ni "Kilimo Kwanza". Serikali itaweka mkazo katika kupanua na kuboresha kilimo kwa mapana yake (mazao, mifugo, uvuvi, mazao ya misitu na nyuki, uwindaji, umwagiliaji, ushirika na masoko), ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo (mbolea na madawa), uzalishaji wa mbegu bora, upatikanaji wa zana za kilimo, huduma za ugani na mikopo nafuu kwa ajili ya kilimo. Aidha, Serikali itatilia mkazo katika kuendeleza na kupanua miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Vile vile ufugaji utaendelezwa kwa kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, malisho, machinjio ya mifugo na kuendeleza viwanda vya kusindika nyama. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa chakula cha kutosha kinapatikana nchini, pamoja na kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kikao cha wadau wa kilimo kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 2 – 3 Juni 2009, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali imeamua kukipa kipaumbele kilimo katika mapana yake kwa kuandaa nguzo kumi za mapinduzi ya kilimo *(Ten Pillars of a Green Revolution in Tanzania*) ambazo

ni Dira ya Kilimo Kwanza; Ugharimiaji wa Kilimo Kwanza; Mabadiliko ya Mkakati wa Kushughulikia Kilimo; Kuhuisha Muundo wa Taasisi za Kilimo; Ardhi; Vivutio vya Kilimo; Mageuzi ya Viwanda vya Kilimo; Sayansi, Teknolojia na Rasilimali Watu; Maendeleo ya Miundombinu; na Uhamasishaji wa Watanzania juu ya dhana ya Kilimo Kwanza. Kikao kilipitia nguzo hizo na kutoa mapendekezo yao. Kwa sasa Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC)* na Shirikisho la Maendeleo ya Sekta Binafsi *(TPSF)*, wanaandaa mpango kazi wa kutekeleza mapendekezo hayo ili kuwasilishwa serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kaulimbiu ya "Kilimo Kwanza", misingi ya malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2009/10 – 2011/12) ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa; kudhibiti kasi ya upandaji bei; na kutengemaza viwango vya ubadilishanaji fedha;

(ii) Kuimarisha Hifadhi ya Chakula ili kuweza kununua mazao ya kutosha kulingana na mahitaji ya Taifa. Aidha, mikoa sita ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Morogoro na Kigoma inayozalisha mazao ya chakula kwa wingi, itapewa kipaumbele katika kupatiwa pembejeo za kilimo;

(iii) Kuendeleza sekta ya kilimo kwa kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo kama mbolea, mbegu bora na dawa za kuua wadudu; kuongeza thamani na ubora wa bidhaa za kilimo na upatikanaji wa masoko; kuendeleza viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo; kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji na kuhimiza matumizi endelevu ya skimu za umwagiliaji; kuongeza upatikanaji wa mikopo ya kilimo na yenye gharama nafuu; na kuimarisha ufanisi na upatikanaji wa huduma za ugani;

(iv) Kuendeleza mifugo ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, majosho na machinjio ya mifugo; kuboresha huduma za ugani na upatikanaji wa maeneo ya ufugaji; kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa kisasa kwa wafugaji; kudhibiti magonjwa ya mifugo; kuimarisha viwanda vya nyama na maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa;

(v) Kuendeleza uvuvi, kuboresha zana za uvuvi na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kuhifadhi samaki;

(vi) Kutekeleza miradi muhimu ya miundombinu ikijumuisha reli, barabara, bandari, nishati na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Miradi hii inajumuisha miradi ya kikanda ya Ukanda wa Kaskazini - Kusini unaounganisha ukanda wa shaba wa Zambia na DRC na Ukanda wa Kati (Dar es Salaam – Isaka – Rwanda – Burundi). Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu zinaendelea. Aidha, mradi mwingine ni mradi wa umeme utakaounganisha Tanzania, Kenya na Zambia kupitia Sumbawanga. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zinatafutwa;

(vii) Kuchukua hatua za kuimarisha mashirika ya umma kama vile ATCL, TRL na TPA, kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na mashirika hayo;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya ukuaji wa sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuendeleza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) hasa katika maeneo ya miundombinu na utoaji huduma kama vile za afya, maji na elimu. Sera ya PPP inakamilishwa na Serikali mwishoni mwa mwaka huu wa fedha (2008/09);

(ix) Kuchukua hatua za kurahisisha taratibu za kuwekeza na kufanya biashara nchini ili kuwapunguzia urasimu wawekezaji wa ndani na nje;

(x) Kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta za kijamii na kuboresha utoaji huduma, ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuboresha shughuli za ukaguzi na usimamizi wa elimu na kuboresha utoaji wa huduma za afya; na

(xi) Kuboresha sekta ya utalii kwa kuhamasisha utalii wa ndani, kutangaza vivutio vya utalii wetu nje; na kutafuta masoko hususan nchi za Asia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msukosuko katika masoko ya fedha na mitaji na athari zake katika uchumi duniani, uchumi wa Tanzania nao umeanza kuathirika, hususan katika maeneo muhimu ya kilimo, utalii, madini na uwekezaji. Mheshimiwa Rais jana alizungumzia kwa kirefu lakini pia na mimi niongezee kidogo. Athari za msukosuko huu zinatarajiwa kuwa za mpito na hivyo uchumi wetu unatarajiwa kuimarika tena katika kipindi cha muda wa kati. Kwa kuzingatia hayo, malengo ya sera za uchumi jumla katika mwaka 2009/10 - 2011/12, yatakuwa yafuatayo:-

(i) Pato Halisi la Taifa litakua kwa asilimia 5.0 mwaka 2009, asilimia 5.7 mwaka 2010 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2011 na asilimia 7.5 mwaka 2012;

(ii) Kasi ya upandaji bei itapungua na kufikia chini ya asilimia 10 mwishoni mwa Juni 2010;

(iii) Mapato ya ndani yataongezeka kufikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 15.9 mwaka 2008/09; asilimia 16.4 mwaka 2009/10; asilimia 17.2 mwaka 2010/11; na asilimia 18.3 mwaka 2011/12;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) katika wigo utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei na kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(v) Kuwa na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha za nje kati ya mabenki; na

(vi) Kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo katika sekta ya fedha, ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 5.0 mwaka 2009 kutokana na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani ambao nimeeleza hapo awali, kutaathiri malengo tuliyokuwa tumejiwekea ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Hivyo, ili kujinasua katika hali hiyo, tunalazimika kuchukua hatua za ziada, hususan katika sekta za kilimo na miundombinu ambayo ndiyo maeneo yatakayoweza kuchochea ukuaji wa uchumi kwa haraka na hivyo kuturudisha katika malengo yetu ya awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo ya mpango na bajeti kwa kipindi cha 2009/10 – 2011/12, napenda kusisitiza mambo muhimu ambayo tunahitaji kuyapa kipaumbele katika utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu kwa mwaka 2009/10 kama ifuatavyo:-

(i) Kukabiliana na athari zinazotokana na msukosuko wa uchumi duniani;

(ii) Kuongeza uwekezaji katika maeneo yenye mwingiliano kisekta hususan kilimo, miundombinu, uzalishaji viwandani na nishati na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika maeneo hayo;

(iii) Kuongeza upatikanaji wa mikopo hasa kwa sekta ya kilimo kwa kuanzisha benki ya kilimo na ya wanawake;

(iv) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula;

(v) Kuongeza na kuboresha mapato ya ndani ili kuweza kugharimia sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali na kuimarisha usimamizi katika matumizi ya fedha za umma;

(vi) Kuboresha mipango ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; na

(vii) Kukamilisha upimaji wa ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza kuwa, Tanzania inazo rasilimali nyingi ambazo kama tukiweza kuzitumia ipasavyo, zinaweza kutusaidia kuondoa matatizo mengi ya kiuchumi na kijamii yanayotukabili. Kwa hiyo, unahitajika umakini zaidi katika matumizi ya rasilimali tulizonazo ili kuweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa haraka zaidi. “Kilimo Kwanza” ndio kaulimbiu ya Serikali kwa mwaka 2009/10 kama nilivyosema hapo awali. Tunatarajia kuiimarisha Benki ya Rasilimali na kufungua dirisha la mikopo ya kilimo katika benki hiyo na hatimaye kuanzisha Benki ya Kilimo na kuhakikisha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu na zana na pembejeo za kilimo kwa wakati kama Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alivyosema jana. Vile vile hatua zitachukuliwa kunusuru maeneo yaliyoathirika na msukosuko wa kiuchumi hususan katika mazao, utalii na mabenki. Kadhalika, Serikali itaendelea na jukumu la kuwawezesha na kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kuelekeza rasilimali tulizonazo ili tuwe na maendeleo yenye kuwiana katika kila ngazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa kulielezea Bunge na Taifa, hali ya uchumi wa Taifa letu na mipango ya baadaye kwa ufasaha mzuri.

Waheshimiwa wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kuhusu mpango wa uchumi imetolewa na imeungwa mkono, lakini kwa utaratibu uliomo katika Kanuni, hoja hii hamuwezi kuiamua hadi msikie na hoja ya bajeti ambayo ndiyo itafuata saa 10.00 alasiri.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 10.00 alasiri.

*(Saa 6.45 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010**

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Pamoja na hotuba hii, vipo vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kitabu cha Kwanza, kinahusu makisio ya mapato na kinajumuisha hatua mpya za kodi ambazo hutangazwa wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti. Kitabu cha Pili na cha Tatu ni vya makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya. Kitabu cha Nne, kinaelezea makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, pamoja na Halmashauri. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2009, ambao ni sehemu ya Bajeti hii pia umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Bajeti yamehusisha Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali na wadau wengine. Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia walipata fursa ya kujadili Mwongozo wa Mpango na Bajeti mapema mwaka huu. Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali ni hatua muhimu katika maandalizi ya bajeti kwa kuwa unatoa fursa kwa wadau na hasa Waheshimiwa Wabunge kutoa michango yao mapema kabla mapendekezo ya bajeti hayajakamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa rasmi. Kwa niaba ya Serikali, nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa maoni yao ambayo yamezingatiwa katika bajeti hii. Utaratibu huu utakuwa ni endelevu na tutautumia kwa pamoja katika kuweka mikakati itakayoharakisha utekelezaji wa ahadi ya Chama Tawala ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati, wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuchambua mapendekezo ya Bajeti kwa undani na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali ya Bajeti hii. Ushauri wa Kamati hii, umesaidia katika kuboresha Bajeti ninayoiwasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Wizara zote, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya, Taasisi za Kitaifa na Kimataifa na Wawakilishi wa Sekta Binafsi, kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya Bajeti hii. Naomba niishukuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009 na nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Uchumi, nikianza na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Jeremia S. Sumari (Mbunge) na Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee (Mbunge); Katibu Mkuu, Ramadhani M. Khijjah, Naibu Makatibu Wakuu; John M. Haule, Laston T. Msongole na Dkt. Philip I. Mpango; Wakuu wa Idara; na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Vile vile namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mwisho, nawashukuru kipekee wataalamu na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu sera, mikakati na masuala mbalimbali ya kodi, ambayo yamezingatiwa kwa kiasi kikubwa katika kuandaa Bajeti hii. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Rais

Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonayo kwangu kwa kunikabidhi madaraka makubwa ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, nitayatekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uwezo na ujuzi wangu wote. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa hotuba nzuri aliyoitoa kwa Wazee wa Dodoma, ambayo kwa kiasi kikubwa imerahisisha kazi yangu ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2009/10, imeandaliwa wakati ambapo dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi, ambao kwa kiwango fulani, umeathiri uchumi wetu na vyanzo vya mapato yetu ya ndani. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania, imejitahidi kutengeneza mazingira yatakayosaidia upatikanaji wa vyanzo vingine vya mapato ili kuziba pengo lililotokana na upungufu wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilitoa muhtasari wa mwenendo wa hali ya uchumi wa nchi katika kipindi cha mwaka 2008 na malengo ya uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2009/10 – 2011/12). Sasa napenda nitoe maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti ya mwaka 2008/09 katika kipindi cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na misingi ya sera nilizozieleza katika Bunge hili mwaka jana. Sera hizo zililenga katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kusimamia matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji. Aidha, Serikali ilikusudia kuendelea kudhibiti ongezeko la Deni la Taifa, pamoja na kuboresha mahusiano na wahisani wanaosaidia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kutekeleza bajeti ya mwaka 2008/2009, mambo kadhaa yamejitokeza ikiwa ni pamoja na yafuatayo: -

(i) Msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani umeanza kuathiri uchumi na Bajeti ya Serikali. Sekta zilizoathirika zaidi ni kilimo, viwanda, madini na utalii. Serikali inachukua hatua kukabiliana na hali hiyo. Aidha, kamati maalumu iliyoundwa chini ya Uenyekiti wa Gavana wa Benki Kuu, ikijumuisha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Wataalamu kutoka pande zote mbili za Muungano, imeshatoa mapendekezo yake ambayo yanafanyiwa kazi na Serikali. Baadhi ya mapendekezo hayo yamejumuishwa katika Bajeti hii kama nitakavyoyaeleza hapo baadaye;

(ii) Kutokana na msukosuko wa kifedha na kiuchumi unaoendelea duniani, mwenendo wa makusanyo ya mapato umekuwa si wa kuridhisha katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka 2008/09 na mwelekeo ni kwamba, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2008/09, mapato hayatafikia lengo kwa asilimia 10;

(iii) Bado ulipaji kodi unagusa sehemu ndogo ya uchumi na hivyo kuwa chini ya mapato yanayoweza kukusanywa. Serikali inaendelea kuchukua hatua ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato; na

(iv) Uhaba wa chakula umeanza kujitokeza katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Hatua zinachukuliwa ili kukabiliana na tatizo hili, ikiwa ni pamoja na kusafirisha mazao ya chakula kutoka maeneo yenye ziada kupeleka maeneo yenye uhaba.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/09, Serikali ilikusudia kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi milioni 4,728,595 (trilioni 4.7), sawa na asilimia 18.5 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 16.7 mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa katika kujenga uwezo endelevu wa kukusanya mapato ya ndani ili kugharimia matumizi yote ya kawaida ni pamoja na:-

(i) Kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara;

(ii) Kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Mamlaka ya Mapato *(TRA Third Five-Year Corporate Plan 2008/09–2012/13)* ili kuongeza uwajibikaji miongoni mwa walipa kodi na watoza kodi kwa lengo la kuweka mkazo katika ufanisi wa ukusanyaji kodi;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa ushuru na kodi kwenye Idara ya Forodha;

(iv) Kuboresha taratibu za kukusanya mapato yasiyo ya kodi; na

(v) Kuboresha Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo na hatua nyingine za mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Sura ya 148. Marekebisho haya ni pamoja na kupanua wigo wa huduma zinazotozwa asilimia sifuri ya *VAT* zinapokuwa zimetolewa kwa watumiaji wa nje ya nchi (*export of services*). Hatua hii ilikusudia kutoa motisha zaidi katika ukuzaji wa biashara ya kimataifa katika huduma na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya huduma katika Pato la Taifa; kusamehe *VAT* kwenye mafuta mazito yanayotumika kama nishati ya kupikia na kusamehe *VAT* kwenye gesi asilia iliyosindikwa (*Compressed Natural Gas* - *CNG*) na mitungi ya kuhifadhia gesi hiyo ili kulinda mazingira; kusamehe *VAT* kwenye lami (*Bitumen*) ili kupunguza gharama za matengenezo ya barabara; na kutoza *VAT* kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye magunia yanayotengenezwa hapa nchini ili kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo na kutoa unafuu wa bei kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/09, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kwa kuanzisha kodi mbadala ya mapato ya mauzo ghafi *(gross turnover)* kwa kampuni zinazoonesha kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Aidha, makampuni haya hupata faida ya kibiashara *(commercial profits)*, lakini katika kukokotoa faida inayostahili kulipiwa kodi zinaonesha hasara (*tax loss)* inayosababishwa na vivutio vya uwekezaji ikiwemo viwango vikubwa vya punguzo la gharama za mitaji (*capital expenses*) vinavyoruhusiwa kisheria; Serikali pia ilifanya marekebisho kwenye ada za magari kwa kupunguza viwango vya ada ya mwaka ya leseni za magari na kusamehe ada ya mwaka ya leseni kwa matrekta ya kilimo. Aidha, kwa upande wa Kodi ya Majengo, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Manispaa za Dar es Salaam, ilipewa jukumu la kukusanya kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama, walikubaliana kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Forodha kwa kusamehe ushuru wa forodha kwenye mali ghafi na vifaa vinavyoagizwa na kampuni ya *TANELEC* kwa ajili ya kutengeneza mashine za kuongeza na kupunguza nguvu ya umeme (*transformers and switch gears);* kusamehe ushuru wa forodha kwenye majembe ya mkono pamoja na pembejeo nyingine zote za kilimo zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, mapato ya ndani yaliyokusanywa yalikuwa shilingi milioni 3,199,134 (trilioni 3.2), sawa na asilimia 91 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 3,529,214 (trilioni 3.5). Huu ni upungufu wa shilingi milioni 330,080 ikilinganishwa na lengo. Mwenendo huu usioridhisha umetokana na baadhi ya vyanzo vya kodi kutofanya vizuri. Vyanzo hivyo ni pamoja na Ushuru wa Bidhaa zinazozalishwa nchini, ambapo makusanyo halisi yalifikia shilingi milioni 222,737, sawa na asilimia 85 ya makadirio ya kukusanya shilingi milioni 262,460 katika kipindi hicho. Aidha, makusanyo kutokana na vyanzo vya kodi ya mapato yalikuwa shilingi milioni 940,675, ikiwa ni asilimia 89 ya lengo. Serikali ilipanga kukusanya shilingi milioni 435,225 kwenye ushuru wa bidhaa za nje, lakini imekusanya shilingi milioni 343,331, sawa na upungufu wa asilimia 21. Maeneo ambayo yamefanya vizuri ni Kodi ya Ongezeko la Thamani ambayo yalifikia shilingi milioni 490,662, ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya shilingi milioni 488,461. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi ikiwa ni pamoja na yale yanayokusanywa na Wizara, Idara na Mikoa yalifikia shilingi milioni 138,479 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya shilingi milioni 184,988 na hivyo kuwa na upungufu wa asilimia 25 ya makadirio. Upungufu huu unatokana hasa na kusitishwa kwa muda, uvunaji wa misitu na upungufu wa samaki katika Ziwa Victoria. Aidha, uamuzi wa kusimamisha kwa muda utoaji wa leseni za uchimbaji wa madini, umechangia upungufu wa mapato kutoka vyanzo hivyo. Kwa upande wa mapato yatokanayo na ubinafsishaji, kiasi cha shilingi bilioni 45 zilipatikana katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, sawa na makadirio katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendeleza sera ya kutokukopa kutoka vyombo vya fedha kugharamia bajeti yake hasa matumizi ya kawaida. Hata hivyo, dhamana za Serikali zenye thamani ya shilingi milioni 559,600 ziliuzwa katika soko ili kulipia zile zilizoiva (*rollover*) na kusaidia kudhibiti ujazi wa fedha. Kwa kipindi kilichoishia Machi 2009, Serikali ilikuwa na akiba Benki Kuu ya shilingi milioni 186,854.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134 na Kanuni zake, imeendelea kuwa msingi na nguzo kuu za ukopaji mikopo nafuu, utoaji dhamana na kupokea misaada ikiwemo unafuu wa madeni. Kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa, nchi yetu ni miongoni mwa baadhi ya nchi za Afrika ambazo zimeweza kudumisha uchumi tulivu, deni letu linahimilika na tunakopesheka. Aidha, Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA), umekuwa Dira na Mwongozo unaokubalika na Wahisani wetu katika kuendelea kupatikana na kuongezeka kwa misaada katika Mfumo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jumla ya misaada na mikopo ya bajeti *(General Budget Support - GBS)* katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi, 2009 ilikuwa shilingi milioni 869,563, ambazo ni sawa na asilimia 115 ya makadirio ya shilingi milioni 757,722 katika kipindi hicho.

Hii inatokana na baadhi ya Wahisani kutoa misaada na mikopo zaidi ya makadirio ya awali, pamoja na kushuka kwa thamani ya sarafu yetu dhidi ya Dola ya Kimarekani, ikilinganishwa na makadirio ya awali. Aidha, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo (ikijumuisha Mifuko ya Kisekta - Basket Funds), kwa kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, ilifikia shilingi milioni 867,564, sawa na asilimia 59 ya makadirio kwa mwaka 2008/09. Vile vile jumla ya shilingi milioni 6,677 zilipatikana kutoka Marekani chini ya

Programu ya MCC.  Pia shilingi milioni 43,806 za misamaha ya madeni *(MDRI)*, zilitumika katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwianisha matumizi na malengo ya kisera kama yalivyoainishwa katika MKUKUTA. Aidha, utaratibu wa kutumia kadiri tunavyopata, umeendelea katika mwaka huu wa fedha na umesaidia sana katika kupanga matumizi yetu. Jumla ya matumizi halisi katika kipindi cha Julai 2008 - Machi 2009 yalikuwa shilingi milioni 4,657,893 (trilioni 4.7), sawa na asilimia 87 ya makadirio ya shilingi milioni 5,364,868 (trilioni 5.4) katika kipindi hicho.  Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 3,142,301 (trilioni 3.1) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 1,515,592 (trilioni 1.5) ni matumizi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai 2008 – Machi 2009, yalikuwa shilingi milioni 1,237,171 (trilioni 1.24), sawa na asilimia 102 ya makadirio ya shilingi milioni 1,211,586 (trilioni 1.21) kwa kipindi hicho. Sababu ya ongezeko hili ni kujumuishwa kwa malipo ya marekebisho ya ongezeko la mishahara ya watumishi wa Serikali, pamoja na malimbikizo ya mishahara ya miezi sita kutoka Januari hadi Juni, 2008 yaliyolipwa mwezi Agosti, 2008.

Mheshimiwa Spika, malipo ya riba kwa madeni ya ndani katika kipindi cha Julai 2008 - Machi 2009, yalifikia shilingi milioni 144,080, sawa na asilimia 106 ya lengo la kulipa shilingi milioni 135,561 katika kipindi hicho. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa malipo ya riba kutokana na malimbikizo ya madeni ya ndani. Kwa upande wa madeni ya nje, kiasi cha shilingi milioni 24,350 zilitumika kulipia riba. Ongezeko hilo limetokana na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania, ikilinganishwa na Dola ya Kimarekani. Kwa ujumla, matumizi ya madeni mengine yalikuwa ni shilingi milioni 284,320 ikiwa ni asilimia 106 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri katika kipindi cha Julai 2008 - Machi 2009, yalifikia shilingi milioni 1,452,380 (trilioni 1.45), sawa na asilimia 86 ikilinganishwa na makadirio kwa kipindi hicho. Mwenendo wa matumizi umekuwa chini kutokana na makusanyo kuwa chini ya malengo kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuboresha usimamizi wa Bajeti, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa watendaji katika Kitengo cha Kusimamia Mwenendo wa Fedha za Serikali *(Cash Management Unit)* katika Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na Maafisa Mipango na Bajeti katika Wizara, Idara, Taasisi na Serikali za Mitaa, ili kuboresha mipango na kusimamia vyema utekelezaji wa Bajeti. Kamati ya Kusimamia Fedha za Serikali *(Cash Management Committee)*, inasimamia kwa karibu mwenendo wa mapato na matumizi kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali unawiana na sera za fedha.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yamepatikana katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.  Hii inajidhihirisha katika maeneo yafuatayo:  Kuundwa kwa kitengo maalumu cha kusimamia ununuzi na kitengo cha ukaguzi katika kila Wizara, Idara na Taasisi; kuundwa kwa Kamati za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali *(Audit Committees);* na kuimarishwa kwa Kamati za Bunge za Mahesabu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa (PAC na LAAC), kwa kupatiwa mafunzo nje na ndani ya nchi. Aidha, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuunda idara inayojitegemea ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali *(Internal Auditor's General Department*). Mkaguzi huyu atakuwa na mamlaka ya kusimamia ukaguzi wa ndani

wa hesabu za Serikali kwa ujumla na atawajibika moja kwa moja kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mabadiliko ya Mfumo wa Takwimu za Fedha za Serikali *(Government Finance Statistics – GFS),* kutoka mfumo wa *GFS 1986* na kwenda *GFS 2001* ili kuendana na mabadiliko yaliyofanywa na Shirika la Fedha la Kimataifa tangu mwaka 2001. Mabadiliko hayo yana lengo la kuweka mfumo unaofaa kwa uchambuzi na tathmini ya Sera za Bajeti, hususan utendaji wa Serikali na sekta ya umma kwa mapana yake *(Broader Public Sector).* Hivyo, vitabu vyote vinne vya bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/10, vimeandaliwa kwa mfumo wa *GFS 2001*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali imeanzisha Kitengo cha Sera za Ununuzi wa Umma ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuimarisha shughuli za Ununuzi wa Umma. Kitengo hiki kinalenga kutoa mchango wa kitaalamu katika kubuni, kuendeleza na kuzifanyia marekebisho sera, sheria, kanuni, nyaraka na miongozo ya ununuzi wa umma, ikiwa ni pamoja na kutathmini utekelezaji mzima wa Sera ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kwa mwaka 2007/2008, inaonesha kuimarika kwa udhibiti na usimamizi wa fedha hasa katika Wizara na Idara za Serikali Kuu, hivyo kupungua kwa hoja za ukaguzi wa fedha za umma. Serikali inatambua kuwa bado usimamizi haujafikia hali ya kuridhisha hasa katika Serikali za Mitaa, ambako hali ya udhibiti inahitaji kufanyiwa kazi kubwa ili iweze kuwa katika hali ya kuridhisha. Hali hii pia inaonekana katika Taarifa za Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa (PAC na LAAC), ambazo nazo zimeonesha udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali, udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma umejitokeza zaidi katika maeneo yafuatayo: Nyaraka za malipo kutokuwa na viambatisho vya kutosha ili kuthibitisha usahihi na uhalali wa malipo; kutozingatia sheria na kanuni za ununuzi; masurufu ya kazi na safari kutorejeshwa kwa wakati kwa mujibu wa sheria na kanuni; kutopatikana kwa nyaraka za baadhi ya miradi ya Wahisani *(Direct to Projects Funds),* hivyo kushindwa kuoanisha bajeti iliyopitishwa na Bunge na matumizi halisi; kushindwa kukusanya maduhuli kama ilivyoidhinishwa katika bajeti; na kutokuthamanisha mali za Serikali zisizohamishika.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua matatizo yaliyoonekana kwenye Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na zile za Kamati za Bunge za Hesabu, Serikali itachukua na kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa Maafisa Masuhuli wote na watendaji wao kuhusu taratibu za usimamizi wa fedha za umma ili kuwawezesha kuelewa vyema na kuzisimamia sheria na kanuni zinazoongoza matumizi ya fedha na mali za umma.

(ii) Kuhakikisha kila taasisi ya umma inakuwa na bodi ya zabuni na kuwapatia mafunzo wajumbe wote wa bodi hizo ili kuboresha utendaji wao.

(iii) Kuchukua hatua zitakazoimarisha viwango vya ukaguzi wa ndani kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi, kuimarisha ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit),* kufuatilia kwa karibu matumizi ya Serikali *(Expenditure Tracking),* pamoja na

kuhakikisha kuwa Idara itakayoanzishwa ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali inafanya kazi zake kikamilifu.

(iv) Kuimarisha ukaguzi wa awali *(pre-audit)* katika kila Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa.

(v) Kuboresha kamati za ukaguzi ili kuziwezesha kufanya kazi zake kwa uhuru na ufanisi zaidi; na

(vi) Kukamilisha zoezi la kuthamanisha mali za Serikali katika Wizara 20 kwa lengo la kuziweka katika daftari la kudumu. Baada ya zoezi hili kukamilika kwenye Wizara hizi, mchakato utaendelea katika Wizara nyingine zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafungu katika Wizara na Halmashauri, yamefanya vizuri na hivyo kupata hati safi za ukaguzi. Mafungu husika yanastahili pongezi. Serikali itaendeleza juhudi zitakazoimarisha zaidi usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Matokeo ya juhudi hizo yataonekana katika kuimarika kwa huduma za jamii zinazotolewa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali Kuu imeendelea kupeleka fedha katika Serikali za Mitaa ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kama yalivyopangwa kwenye bajeti. Hadi kufikia Machi 2009, Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 1,121,134 (trilioni 1.1). Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 914,746 ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha mishahara na shilingi milioni 206,387 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Serikali imefanya juhudi katika kuajiri wahasibu na wakaguzi wa hesabu za ndani katika Serikali za Mitaa ili kuboresha usimamizi wa fedha katika ngazi hiyo. Katika mwaka 2008/09, jumla ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu 202 waliajiriwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi (*Decentralisation by Devolution – D by D)* upo katika mwaka wake wa tatu. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na baadhi ya Wizara kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu majukumu yao katika Serikali za Mitaa; Serikali za Mitaa zimeboresha uwajibikaji na usimamizi wa ununuzi; na kuimarisha mipango ya bajeti shirikishi. Pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto zinazokabili utekelezaji wa Sera ya *"D by D"* ikijumuisha kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote; kujenga uwezo wa watendaji katika Serikali za Mitaa ili kuweza kuimarisha zaidi uwajibikaji na usimamizi wa fedha za Serikali; na kuziwezesha Halmashauri zilizo katika mazingira magumu kuweza kuajiri na kuwabakisha watendaji wenye uwezo katika maeneo yao kwa kuweka mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha inaendelea na jukumu lake la kuzishauri Serikali zote mbili; SMZ na SMT. Baada ya kumaliza kipindi cha kwanza cha Tume, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameteua Wajumbe wapya wa Tume hiyo. Aidha, Serikali zote mbili zimekamilisha uchambuzi wa Taarifa za Tume na sasa zipo kwenye taratibu za kupatiwa maamuzi na Serikali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza ushirikiano baina ya Wizara za Fedha na Uchumi SMT na SMZ, mambo kadhaa yamefanyika ikiwa ni pamoja na kuihusisha SMZ katika masuala ya kifedha yanayohusisha Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika; kujenga uwezo kwa wataalamu wa fedha wa SMZ katika kuratibu fedha za nje; na kubadilishana uzoefu katika uandaaji wa Bajeti. Aidha, kufuatia

majadiliano ya pande mbili, makubaliano yamefikiwa ya kuipatia SMZ asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti kuanzia mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 katika malengo yake makuu ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi; kuboresha mfumo wa utawala wa kodi; kurekebisha sheria, kanuni, leseni na huduma nyingine za Serikali ili ziendane na dhana ya uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko; kurahisisha upatikanaji wa mitaji na kuwezesha wananchi kuwa wenye kukopesheka. Malengo mengine ni kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu; kuimarisha miundombinu; kuboresha mazingira yatakayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ubinafsishaji wa mashirika ya umma; kuimarisha uwezo wa kuzalisha bidhaa bora, kutoa huduma kwa ufanisi, usanifu na ustadi wa kiwango cha juu na kutafuta masoko; na kutumia ardhi kama chombo cha kuweka chachu ya uwezeshaji. Sera hii inatekelezwa na sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hii ni pamoja na kukua kwa Pato Halisi la Taifa; kukua kwa Pato la Wastani la kila Mtanzania; kupungua kwa umaskini wa mahitaji ya msingi *(Basic Needs);* kuanzishwa kwa mifuko mbalimbali ili kurahisisha upatikanaji wa mitaji; na mashamba na viwanja vimepimwa ili hati zitumike kama dhamana ya kuombea mikopo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2009, mafanikio yalipatikana katika utekelezaji wa baadhi ya mifuko ya uwezeshaji kama Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kwa kutoa mikopo nafuu ya shilingi bilioni 42.48, ikilinganishwa na shilingi bilioni 31.0 zilizokadiriwa hapo awali. Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi na Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo (*SELF*), kwa pamoja ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 68.58 kwa wajasiriamali 131,640 kupitia SACCOS 210 na Vikundi 86. Kati ya wajasiriamali hao, wanawake ni 58,907 na wanaume 72,633.

Aidha, mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa watendaji wapatao 1,889 kutoka katika asasi ndogo za fedha zikiwemo SACCOS 328 na mashirika yasiyo ya kiserikali. Pia uhamasishaji wa wajasiriamali kujiunga katika SACCOS ulifanyika na kufanikiwa kuongeza idadi ya SACCOS kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi SACCOS 4,780 mwaka 2008. Vile vile huduma ya mikopo midogo midogo imekuwa ikitolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).*

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya utekelezaji wa MKUKUTA inaonesha kwamba, mafanikio kadhaa yamepatikana katika maeneo yake yote matatu ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji. Hata hivyo, kasi ya kupungua kwa umaskini hairidhishi. Kwa sababu hiyo, Serikali imedhamiria kuchukua hatua za kuongeza kasi ya kupunguza umaskini hasa kwa kuboresha uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Aidha, katika eneo la ustawi wa jamii, mafanikio yamepatikana kwenye elimu katika ngazi zote, japokuwa kumekuwa na matatizo ya upungufu wa walimu, vifaa vya kufundishia na miundombinu yake. Kuhusu afya, mafanikio yamepatikana katika afya ya msingi, ingawa hatujaweza kupunguza vifo vya uzazi na watoto kwa kiwango kikubwa. Serikali itaendelea kuchukua hatua kukabiliana na matatizo haya hasa kupitia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuboresha Afya ya Msingi. Upatikanaji wa maji mijini na vijijini umeongezeka kiasi na hivyo kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi hasa akina mama na watoto. Hata hivyo, bado ipo changamoto ya kufikisha huduma hii muhimu karibu zaidi na wananchi hasa vijijini. Katika eneo la utawala bora na uwajibikaji, vyombo

vinavyohusika na haki za binadamu, vimefanya kazi nzuri hadi sasa na vitaendelea kuongezewa uwezo wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya MKUKUTA itafikia mwisho wake mnamo mwezi Juni 2010. Tayari Serikali imeanza kazi ya kuandaa awamu ya pili ya MKUKUTA. Serikali itatumia uzoefu uliopatikana katika awamu ya kwanza ya MKUKUTA wakati wa kuandaa awamu ya pili. Lengo ni kuepuka upungufu uliojitokeza katika kutekeleza awamu ya kwanza hasa katika maeneo ya kipaumbele, upatikanaji na ugawaji wa rasilimali, usimamizi, ufuatiliaji na kufanya tathmini ya mara kwa mara ya utekelezaji na upatikanaji wa taarifa kwa wakati. Marekebisho haya ni muhimu ili kufanya utekelezaji wa awamu ya pili ya MKUKUTA ufanikishe azma ya kuongeza kasi ya kupunguza umaskini na hivyo kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. MKUKUTA II utaanza kutekelezwa Julai 1, 2010. Hivyo, ni matumaini yetu kuwa, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, watashiriki kikamilifu na kutoa michango yao katika mchakato huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mwenendo wa bajeti kwa miezi tisa ya mwaka 2008/09, inaonesha kuwa malengo ya sera za mapato hayatofikiwa kama ilivyopangwa. Mapato ya ndani yanategemewa kufikia shilingi milioni 4,248,858 (trilioni 4.2), ikiwa ni asilimia 90 ya lengo la shilingi milioni 4,728,595 (trilioni 4.7). Upungufu huu unatokana na msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani, uliojitokeza hasa katika nusu ya pili ya mwaka 2008, ambao umeathiri taasisi na makampuni mbalimbali na hivyo kushindwa kulipa kodi kama ilivyotarajiwa. Kuathirika kwa ufanisi wa kodi kumeonekana kwa walipa kodi wakubwa, ambao kodi zao zina mchango mkubwa katika makusanyo. Aidha, misaada na mikopo kutoka nje inategemewa kupatikana kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, tunakadiria kwamba, hadi kufikia Juni 2009, matumizi ya Serikali yatafikiwa kama yalivyopangwa kwa kuwa upungufu uliojitokeza kwenye mapato utafidiwa na ongezeko la mikopo na misaada ya kibajeti, pamoja na kuuza hatifungani za Serikali ambazo hazitachochea mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2009/10 ni ya nne tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani. Misingi na shabaha ya Bajeti hii imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, ambayo inalenga kuwa Tanzania iwe ni nchi yenye kiwango cha kati cha mapato *(Middle Income Country)* na hali bora ya maisha kwa wananchi; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; MKUKUTA; Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini-Tiger Plan 2020)*; na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Tofauti na miaka mingine, Bajeti ya Mwaka 2009/10, itatekelezwa katika mazingira ya msukosuko wa kiuchumi unaoendelea duniani. Ili kukabiliana na hali hii, katika mwaka 2009/10, Serikali imeamua kutoa kipaumbele katika kuboresha kilimo na maeneo yanayosaidia kilimo. Kama nilivyosema leo asubuhi, kaulimbiu ya Serikali kwa mwaka 2009/10 ni “Kilimo Kwanza”. Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kuwa, kilimo kinapatiwa rasilimali zaidi zikiwemo pembejeo na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kuleta maendeleo nchini na maisha bora kwa Watanzania wote, Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2009/10 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa mapato; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali; na kuchukua hatua za kupunguza misamaha ya kodi ili kuongeza mapato.

(ii) Kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana na athari zinazotokana na msukosuko wa kiuchumi duniani.

(iii) Kuboresha na kupanua miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme hasa vijijini.

(iv) Kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa kulinda ajira.

(v) Kujikinga na madhara ya uhaba wa chakula.

(vi) Kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika programu muhimu za kijamii kama vile afya, elimu, maji na kuboresha utoaji wa huduma.

(vii) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa matumizi pamoja na tathmini ya mpango na bajeti ili kuhakikisha rasilimali fedha inatumika kwa ufanisi.

(viii) Kutafuta mikopo zaidi yenye masharti nafuu katika Mashirika ya Kimataifa na kutoka nchi za Mashariki ya Kati na Asia ili kuweza kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na sekta binafsi kwa utaratibu wa *Public-Private Partnership (PPP).*

(ix) Kutenga fedha za kugharimia ukamilishaji wa upimaji wa ardhi ya vijiji 1,500 vilivyobaki.

(x) Kutenga fedha za kugharamia miradi maalumu katika maeneo yenye mazingira magumu yasiyovutia Watumishi kufanya kazi kwenye maeneo hayo; na

(xi) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2009/10, Sera za Mapato zinalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi milioni 5,096,016 (trilioni 5.1), sawa na asilimia 16.4 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na mapato ya asilimia 15.9 ya Pato la Taifa ya mwaka 2008/09. Pamoja na athari za msukosuko wa kiuchumi unaoendelea, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza juhudi za kukusanya mapato ya ndani ili kuweza kugharimia sehemu kubwa ya bajeti kwa mapato ya ndani. Ili kuendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuendelea kupanua wigo wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi na kuendelea kuimarisha uchumi tulivu pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua;

(ii) Kusimamia kwa karibu mageuzi yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato (TRA) chini ya Mpango wake wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano *(Third Corporate Plan)*, ambao malengo yake ni pamoja na kuziba mianya ya ukwepaji kodi; uvujaji wa mapato ya serikali; kuendelea kutoa elimu ya biashara; na namna ya ukokotoaji kodi kwa wafanyabiashara;

(iii) Kuendelea kurekebisha mfumo wa kodi na kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha mifumo ya utendaji;

(iv) Kuendelea kuboresha usimamizi na utendaji katika Idara ya Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na kupunguza mlolongo wa taratibu ndefu ambazo zinawaletea kero walipa kodi;

(v) Kuendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti katika kupeleka mizigo kwenye bandari za nchi kavu *(Inland Container Depot - ICD*), ikiwemo matumizi ya teknolojia ya kisasa;

(vi) Kuimarisha udhibiti wa bidhaa za mafuta ya petroli, ikiwemo kuhakikisha kuwa mita za kupitishia bidhaa hizo *(flow metres*) zinafanya kazi vizuri wakati wote, kushirikiana na Mamlaka husika katika kudhibiti uchanganyaji wa dizeli na mafuta ya taa na kuhakikisha kuwa mafuta yanayopitishwa hapa nchini kwenda nchi jirani *(transit goods)* hayauzwi katika soko la ndani;

(vii) Kuanzisha na kuendesha ghala la forodha kwa ajili ya bidhaa za mafuta (*TIPER Fuel Bonded Warehouse*). Hii itawezesha kuwa na hifadhi ya mafuta, kudhibiti mapato ya Serikali pamoja na kuongeza ufanisi wa soko la bidhaa za mafuta kwa kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kushusha bei kwa watumiaji;

(viii) Kuboresha ukaguzi wa kodi *(field and desk audits*) na usimamizi wa ukusanyaji wa malimbikizo;

(ix) Kuboresha usimamizi wa mapato ya kodi ya majengo na mapato ya kodi yatokanayo na ukodishaji au upangishaji wa majengo hayo; na

(x) Kukamilisha tathmini ya utaratibu na utambuzi wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Mikoa na Idara Zinazojitegemea kwa lengo la kubaini upungufu uliopo na kufanya marekebisho ili kuongeza udhibiti na ufanisi wa makusanyo ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mwongozo utakaowezesha Asasi na Wakala mbalimbali za Serikali zinazotoza kodi ya huduma, kuchangia sehemu ya mapato yao katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vile vile taratibu za kukusanya mapato katika vyanzo vya Wizara na Idara zitaimarishwa ili kuhakikisha kuwa mapato yote yanakusanywa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato kutoka Serikali za Mitaa, mwaka 2009/10 ni wa kwanza kujumuisha mapato hayo kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Hivyo, Bajeti ya Serikali imejumuisha kiasi cha shilingi milioni 138,052 ikiwa ni mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri. Lengo la hatua hii ni kutoa sura kamili ya Bajeti ya Serikali. Mapato hayo yatatumika katika Halmashauri husika na yatatokana na vyanzo vya Halmashauri ambavyo ni pamoja na:-

(i) Ushuru wa huduma, ushuru wa mazao, maegesho, nyumba za kulala wageni, mazao ya misitu, masoko na minada;

(ii) Leseni na vibali ikiwa ni pamoja na leseni za biashara, usafirishaji wa abiria na mizigo; leseni za vileo; na vibali vya ujenzi, kuchimba kifusi, mawe na mchanga;

(iii) Ada na tozo zikijumuisha ada ya masoko, uuzaji wa nyaraka za zabuni, utupaji wa taka na maji taka, ada ya machinjio, minada, ukaguzi na usafirishaji wa wanyama;

(iv) Gawio kutokana na kuwekeza hisa, faida ya biashara za Halmashauri, ukodishaji wa mitambo au mali za kudumu za Halmashauri; na

(v) Mapato ya mirabaha kutokana na maliasili zilizomo katika eneo la Halmashauri pamoja na migodi ya madini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kiwango cha makadirio ya mapato kilichopendekezwa na Serikali za Mitaa, bado Serikali Kuu inaamini kwamba, Serikali za Mitaa zinaweza kukusanya zaidi ya kiwango hiki. Hivyo, Serikali itahakikisha kuwa, inajenga uwezo wa Watendaji wa Serikali za Mitaa kwa kuwapatia utaalamu wa kutosha kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika kukadiria na kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo kutoka nje ni chanzo muhimu cha mapato kwa Bajeti ya Serikali. Katika mwaka 2009/10, Serikali inategemea kupata shilingi milioni 3,181,948 (trilioni 3.18) kutoka kwa Washirika wetu wa Maendeleo, ikiwa ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Kati ya fedha hizi; shilingi milioni 1,193,909 (trilioni 1.19) ni misaada ya kibajeti, shilingi milioni 572,927 ni mifuko ya kisekta na shilingi milioni 1,415,112 (trilioni 1.42) ni kwa ajili ya miradi katika sekta mbalimbali. Kiasi hiki ni ongezeko la shilingi milioni 722,412, sawa na asilimia 30 ya kiwango cha Bajeti ya Mwaka 2008/09. Aidha, baadhi ya Nchi Wahisani na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, wameahidi kuongeza misaada yao kwa Tanzania baada ya kudhihirika kuwa kuna upungufu wa mapato ya ndani na ya nje. Katika kutekeleza hili, Umoja wa Ulaya na Benki ya Dunia, wameahidi kutoa fedha za nyongeza kusaidia kilimo cha mazao ya chakula ili kukabiliana na upungufu.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia pia ipo tayari kutoa fedha za nyongeza kusaidia Bajeti ya Serikali ili kuiwezesha kukabiliana na mahitaji ya ziada ya fedha yatakayotokana na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani. Hivi sasa Serikali inazungumza na Benki ya Dunia kuhusu uwezekano wa mkopo wa nyongeza kwa PRSC 7 kwa kiasi cha Dola za Kimarekani kati ya milioni 100 na 250. Fedha hizi zikipatikana, zitapangiwa matumizi na kuidhinishwa na Bunge kwa utaratibu wa Bajeti ya Nyongeza (*Supplementary Budget*). Vile vile tayari Shirika la Fedha la Kimataifa, kupitia Mpango wake wa *Exogenous Shock Facility (ESF)*, limeidhinisha mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 336 ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni zinazowezesha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Serikali inaendelea kupanua wigo wa kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa kujumuisha Nchi za Mashariki ya Kati na Asia ili kutuongezea uwezo wa kugharimia miradi muhimu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo tunayopata kutoka nje, inalenga katika kuimarisha uwezo wa Serikali kufikisha huduma muhimu kwa wananchi. Ili kufikia azma hii, Serikali itaendeleza juhudi za kuboresha usimamizi na matumizi ya misaada na mikopo kutoka nje kwa kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) na ule wa kusimamia Deni la Taifa. Lengo ni kuhakikisha kuwa, misaada tunayopata ni yenye manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua na kuwashukuru Washirika Wetu Wote wa Maendeleo, kwa misaada yao ambayo imechangia mafanikio yetu katika sekta mbalimbali za uchumi wetu. Naomba niwataje mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo: Belgium, Canada, China, Denmark, United Kingdom, Finland, France, Germany, India, Ireland, Italy, Japan, South Korea, Kuwait, The Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Switzerland, United States of America, African Development Bank, BADEA, European Union, Global Funds, International Monetary Fund, Kuwait Fund, Nordic Fund, Opec Fund, Saudi Fund, United Nations Agencies na The World Bank. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali iliahidi kutokukopa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida. Tanzania kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea, imeathirika na msukosuko wa kiuchumi unaoendelea Duniani. Kutokana na hali hiyo, Serikali inalazimika kutafuta njia mbalimbali za kunusuru uchumi, ikiwa ni pamoja na kukopa kutoka soko la fedha la ndani, bila kuathiri malengo ya uchumi jumla kama vile mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Serikali inakusudia kukopa kiasi cha shilingi milioni 506,193 katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya mapato ya Serikali. Hii inatokana na upungufu unaotarajiwa katika mapato kwa ujumla na kwa kuzingatia kwamba, kuna mahitaji muhimu ambayo hayakwepeki. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 576,476 kitakopwa kwa ajili ya kulipia dhamana zinazoiva. Kiwango hiki cha mikopo ya ndani kinawiana na sera za fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kutekeleza Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa kutekeleza maazimio ya mdahalo wa kitaifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi; kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kwa kuzingatia mahitaji kama ilivyoainishwa katika tafiti mbalimbali; kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi; kuainisha aina za biashara zinazostahili kuendeshwa na Watanzania pekee na zile zinazoweza kuendeshwa kwa ubia na wageni; kuendesha warsha za viongozi wilayani na mikoani ili kueneza, kuelimisha na kuhamasisha wadau juu ya Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na kufuatilia, kuratibu na kutathmini shughuli za uwezeshaji kiuchumi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, utekelezaji wa sera za matumizi utalenga maeneo yafuatayo: Kukabiliana na athari za msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani ili kuunusuru uchumi; kuboresha kilimo na mifugo; kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya kawaida na umwagiliaji; kuendelea kuboresha huduma za elimu na afya, miundombinu, viwanda, utalii na kuendeleza utafiti *(R & D);* kuendelea na utekelezaji wa kupeleka madaraka kwa wananchi *(D by D);* kugharimia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2010 na Sensa ya Watu na Makazi 2012.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni pamoja na kuongeza kima cha chini cha pensheni; kuongeza na kuboresha mtaji wa Benki ya Rasilimali (TIB) kuweza kutoa mikopo kupitia dirisha la mikopo kwa sekta ya kilimo; Serikali kuanzisha Benki ya Kilimo; kupunguza madeni ya mashirika; na kugharimia maandalizi ya kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria. Kwa upande wa maliasili, juhudi zitafanywa kuhamasisha utalii wa ndani na kuvutia watalii kutoka nje; na kuhakikisha upatikanaji wa nishati endelevu na vyanzo mbadala kama vile umeme wa jua, upepo na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kilimo, Mifugo, Maji na Umwagiliaji, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:-

(i) Kuhakikisha kuwa kunapatikana pembejeo za kutosha kwa wakulima na wafugaji ikiwa ni pamoja na mbolea, mbegu bora na dawa. Mkakati mmojawapo ni kuhakikisha kuwa Mfuko wa Pembejeo unatengewa fedha kwa ajili hiyo. Ni muhimu kwa sekta ya kilimo kupatiwa mbolea na mbegu bora kwa wakati;

(ii) Taasisi za utafiti kama vile Ukiliguru, Ilonga, Naliendele na Uyole zitawezeshwa ili kuendeleza kazi zao za utafiti wa mbegu bora. Aidha, taasisi za uzalishaji kama vile Msimba Seed Farm, JKT na Magereza zitapewa jukumu la kuzalisha zaidi mbegu bora zinazotokana na taasisi za utafiti na hivyo wakulima wengi zaidi waweze kunufaika;

(iii) Kuimarisha Hifadhi ya Chakula ili kuweza kununua mazao ya kutosha kulingana na mahitaji ya Taifa. Aidha, mikoa sita ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Morogoro na Kigoma inayozalisha mazao ya chakula kwa wingi itapewa kipaumbele katika kupatiwa pembejeo za kilimo;

(iv) Kuviwezesha vyuo kuandaa maafisa ugani wengi na kuwapatia ajira kwa lengo la kuwasaidia wakulima na wafugaji kuongeza uzalishaji wa mazao na mifugo bora;

(v) Barabara vijijini zitaendelea kuboreshwa kwa lengo la kuimarisha huduma za usafiri vijijini kwa kuwa na usafiri wa uhakika kwa mazao ya wakulima na wafugaji;

(vi) Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo uvunaji wa maji ya mvua kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara;

(vii) Kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji; kuimarisha majosho, malambo, machinjio, ranchi, ubora wa mazao na viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo; na

(viii) Kuboresha vifaa vya kuhifadhia mazao ya kilimo na mifugo, pamoja na kutafuta masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa miundombinu katika shughuli za uzalishaji na maendeleo ya nchi kwa ujumla, Serikali itaendelea kuweka msukumo katika uboreshaji wa barabara, reli, bandari, madaraja na viwanja vya ndege. Katika mwaka 2009/10 maeneo yafuatayo yatazingatiwa:-

(i) Kutekeleza miradi inayoendelea kama vile ya barabara, umeme na maji;

(ii) Kuimarisha mashirika mbalimbali yaliyo na matatizo ikiwa ni pamoja na TTCL, TAZARA, TRL na ATCL kwa lengo la kuongeza ufanisi; na

(iii) Kukamilisha Sera ya Taifa ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi (PPP) ili kuwezesha sekta hiyo kuchangia katika ujenzi wa miundombinu ikishirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za elimu, Serikali itaendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana na kuboresha maeneo yenye upungufu. Kipaumbele kitakuwa ni kuongeza walimu wa kutosha na wenye sifa katika ngazi zote; kuboresha vifaa vya kufundishia na miundombinu; kuimarisha ukaguzi wa elimu kwa ngazi zote nchi nzima; na kujenga na kuimarisha maabara ili kuwawezesha wanafunzi kusoma sayansi. Aidha, Serikali inaandaa mradi mkubwa wa kujenga nyumba za walimu nchi nzima kwa kuanzia na maeneo ya pembezoni yenye mazingira magumu ili kuondoa kero za makazi ya walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za uzazi na mtoto; kuimarisha uwezo wa rasilimali watu katika ngazi zote; kuendelea kukarabati na kujenga vituo vya afya na upatikanaji wa vifaa; kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI; na kuendelea kuboresha Kituo cha Upasuaji Moyo katika Hospitali ya Muhimbili. Lengo la hatua hizo ni kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo ya Milenia yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za maji, Serikali inalenga kupanua na kukarabati miundombinu ya maji safi na umwagiliaji kwa kuboresha usimamizi wa vyanzo vya maji. Aidha, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji-taka mijini utaimarishwa kwa lengo la kutunza mazingira. Katika mwaka 2008/09, mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria - Shinyanga - Kahama uliogharimu fedha za ndani zaidi ya shilingi bilioni 250, ulikamilishwa na usambazaji wa maji katika miji na vijiji unaendelea. Serikali itaendelea kushirikiana na jamii katika kupanga na kutoa miongozo kwa wadau mbalimbali ili kuifanya sekta ya maji kuwa endelevu na ya manufaa kwa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, Serikali itatoa kipaumbele katika uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo kwa kuhusisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya utafiti, Serikali itachukua hatua za kuimarisha vyuo na taasisi za utafiti kwa kujenga uwezo wa kitaaluma na kuongeza idadi ya watafiti, kuanzisha vitovu vya utafiti *(Centres of Excellence)* katika fani mbalimbali ikijumuisha kilimo, misitu, mifugo, uvuvi, maikrobiolojia, teknolojia na sayansi za jamii. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa tafiti hizo zinafanyika kwenye maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kitaifa na kuwa matokeo yake yanatumika katika maendeleo ya viwanda, kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, usafirishaji na ustawi wa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo juu, Bajeti ya Mwaka 2009/10, imezingatia mikakati ya kitaifa inayolenga kuchangia katika kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Mchanganuo wa Bajeti kwa baadhi ya sekta ukijumuisha mishahara ya watumishi wa umma kwa mwaka 2009/10 ni kama ifuatavyo:-

(i) Elimu imetengewa shilingi bilioni 1,743.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,430.4 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 22. Sekta hii bado inaendelea kuchukua sehemu kubwa ya Bajeti kutokana na umuhimu wake;

(ii) Kilimo kimetengewa kiasi cha shilingi bilioni 666.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 513.0 mwaka 2008/09 pamoja na fedha za marejesho za EPA, sawa na ongezeko la asilimia 30. Aidha, Serikali inadhamini mikopo ya Benki kwa Sekta ya Kilimo kupitia vyama vya ushirika na makampuni ya watu binafsi kwa mazao mbalimbali.

(iii) Miundombinu imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1,096.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 973.3 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 12.7;

(iv) Afya imetengewa shilingi bilioni 963.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 910.8 mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 5.7;

(v) Maji imetengewa shilingi bilioni 347.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 231.6 zilizotengwa mwaka 2008/09, sawa na ongezeko la asilimia 50; na

(vi) Nishati na madini imetengewa shilingi bilioni 285.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 378.8 zilizotengwa mwaka 2008/09, sawa na upungufu wa asilimia 24.6. Hali hii imesababishwa na kumalizika mikataba ya kuzalisha umeme kwa makampuni ya kukodi ya Dowans, APR na Aggrekko. Hatua nyingine zinachukuliwa katika mwaka 2009/10 kutafuta mikopo kutoka mashirika ya kimataifa na nchi marafiki ili kuweza kupata rasilimali zaidi za kufanikisha miradi ya nishati nchini. Nchi na mashirika ya fedha ya kimataifa yameonesha nia ya kutusaidia zikiwemo Korea ya Kusini, Saudi Fund, BADEA na OPEC Fund.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo muhimu kwa pamoja yametengewa jumla ya shilingi bilioni 5,103.2, sawa na asilimia 64 ya bajeti yote ya mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza leo asubuhi katika hotuba yangu ya Hali ya Uchumi, dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi ambao athari zake zimejitokeza zaidi katika Sekta za Kilimo, Madini na Utalii. Serikali imechukua hatua mbalimbali za muda mfupi na wa kati katika kukabiliana na msukosuko wa kiuchumi duniani. Hatua hizo zinalenga kupunguza makali au kuhimili shinikizo la msukosuko, hususan kuwalinda wananchi walio katika hatari kubwa zaidi kimaisha; kuboresha mifumo ya dhamana; kuinusuru nchi kutokana na athari za uadimifu wa chakula duniani zilizochochewa na msukosuko pamoja na hali mbaya ya hewa; kulinda programu muhimu za kijamii; na kulinda uwekezaji hasa katika miundombinu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na malengo ya maendeleo ya milenia; kuanzisha utaratibu wa uangalizi na usimamiaji wa mabenki kila siku ili kuweza kubaini matatizo yoyote yatakayojitokeza na kuchukua hatua za haraka. Mikakati mingine ni kuimarisha juhudi za kukusanya mapato ya ndani; kuendelea na kutekeleza mikakati ya kuongeza tija katika sekta ya kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza mfumko wa bei; na kuongeza juhudi za kutangaza vivutio vya utalii hasa utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa ili kukabiliana na athari za msukosuko wa kiuchumi ni pamoja na:-

(i) Kufidia hasara waliyopata wanunuzi wa mazao msimu wa mwaka 2008/09. Mpango huu unajumuisha kufidia vyama vya ushirika na makampuni

yaliyouza bidhaa za pamba na kahawa kwa hasara. Serikali italipa madeni haya moja kwa moja kwenye benki zinazohusika baada ya uhakiki;

(ii) Kutoa udhamini wa kuahirisha mikopo ya waathirika wa msukosuko ambapo Serikali itatoa udhamini kwa mikopo iliyochukuliwa kutoka benki mbalimbali ambayo haijarejeshwa;

(iii) Kutoa mitaji ya uendeshaji kwa riba nafuu. Katika Mpango huu, Serikali itatoa mikopo nafuu kwa mabenki *(Soft Loans)*, ambayo itakopeshwa kwa wenye shughuli zilizokumbwa na msukosuko na hivyo kushindwa kuhimili viwango vya riba vya soko katika msimu ujao;

(iv) Kuboresha mifuko ya kudhamini mikopo ikijumuisha *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)* na *Small and Medium Enterprises (SMEs) Guarantee Scheme.* Hatua hii itasaidia kuongeza dhamana ya mikopo ili kuchochea uzalishaji na mauzo ya bidhaa nje, pamoja na kuongeza mtaji kwenye mfuko wa dhamana kwa SMEs;

(v) Mbali na mchango huu wa Serikali, gharama nyingine zitachangiwa na Benki Kuu ya Tanzania, Benki za Biashara zilizotoa mikopo ambayo kwa sasa ni chechefu na Washirika wa Maendeleo;

(vi) Kutumia fedha za mkopo kutoka Serikali ya India kununulia zana za kilimo kwa nia ya kuboresha uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo. Fedha hizi zitapatikana kufuatia kusainiwa mkataba wa mkopo baina ya Serikali ya Tanzania na India;

(vii) Artumas watakopeshwa fedha ili waweze kuendelea kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa mikoa hiyo;

(viii) Serikali itatafuta mikopo kutoka vyombo vya kimataifa na nchi wahisani ili kugharimia uendeshaji wa shughuli za kampuni ya reli (TRL); na

(ix) Bandari zetu zitatenga gati maalumu kwa ajili ya meli za kitalii pamoja na kuweka huduma husika na mpango utakaozifanya meli hizo zisisubiri bandarini. Hatua hii inalenga kuvutia meli za kitalii kuja nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari nilizozieleza hapo juu, Kamati imebainisha fursa ambazo nchi yetu inaweza kunufaika nazo kutokana na msukosuko huo. Tukizitumia vizuri fursa hizo zinaweza kutuongezea makusanyo ya mapato ya ndani kwa Serikali, kuongeza vipato vya wakulima wetu na hata akiba yetu ya fedha za nje nayo yaweza kuongezeka pia. Kwa muhtasari, fursa kwa nchi yetu zitokanazo na msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani kwa Tanzania ni kama ifuatavyo:-

(i) Tanzania imepakana na nchi kadhaa ambazo hazina bahari (*Land Locked Countries), ambazo* pia zimekumbwa na msukosuko huo. Hivyo, tukiweza kuongeza ufanisi wa bandari yetu ya Dar es Salaam hususan katika kuhudumia shehena za mizigo ya meli hizo, Pato letu litaongezeka. Ni muhimu basi kushughulikia matatizo yanayoikabili Bandari ya Dar es Salaam ikiwemo TICTS;

(ii) Inabidi kubainisha na kupima maeneo ya mashamba makubwa kwa uzalishaji wa mazao ya chakula ili yaweze kutumiwa na wawekezaji katika Sekta ya Kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula na kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje;

(iii) Uhaba wa chakula duniani unatupa fursa ya kuongeza uzalishaji wa chakula hasa katika mikoa sita ya Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma na Morogoro. Hivyo, Serikali itahakikisha kuwa mikoa hiyo inapewa kipaumbele katika kupatiwa pembejeo na zana za kilimo kwa wakati;

(iv) Kutokana na msukosuko kama huo katika nchi za jirani, kuna haja ya kuongeza msukumo zaidi *(aggressiveness)* katika kutafuta masoko katika nchi hizo ili kuweza kuuza mazao ya chakula na bidhaa za viwandani; na

(v) Dirisha la kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania ni fursa nyingine kwa wawekezaji wa ndani katika kilimo. TIB itakuwa na takriban shilingi bilioni 20 kwa ajili hiyo. Taratibu zitaharakishwa ili kuwezesha waombaji wa mikopo wapate mikopo kwa riba nafuu kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari za msukosuko wa kiuchumi unaoendelea duniani, Serikali itachukua hatua za kuboresha ukusanyaji wa mapato. Kama nilivyoeleza hapo awali, hatua hizi zitajumuisha kupanua wigo wa kodi, ikiwa ni pamoja na kurejea sheria na taratibu zinazosimamia misamaha ya kodi kwa nia ya kuipunguza na kudhibiti usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufanyia marekebisho mfumo wa kodi, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine zisizo za kodi chini ya sheria mbalimbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Marekebisho hayo yanalenga kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji hapa nchini ili kupunguza makali ya msukosuko wa uchumi duniani na kurahisisha ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya pia yamezingatia misamaha ya kodi inayotolewa kwa makundi mbalimbali kama vile wawekezaji ikijumuisha sekta ya madini, asasi zisizo za serikali na mashirika ya dini. Tathmini inaonesha kwamba, misamaha ya kodi imekuwa ikiongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka na kufikia wastani wa asilimia 30 ya mapato ya kodi au asilimia 3.5 ya Pato la Taifa katika mwaka 2007/08. Kiwango hiki ni kikubwa ikilinganishwa na viwango vya misamaha inayotolewa na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mathalani, katika nchi ya Kenya misamaha ya kodi inafikia asilimia moja ya Pato la Taifa wakati Uganda ni asilimia 0.4 ya Pato la Taifa. Ongezeko la misamaha linapunguza uwezo wa Serikali kutoa huduma muhimu kama vile miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii na hatimaye kupunguza kasi ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Misamaha ya kodi pia imefungua mwanya wa ukwepaji kodi na hivyo kuvuja kwa mapato. Ili kunusuru hali hii, Serikali inapendekeza kurejea sheria zinazotoa misamaha ya kodi na taratibu za usimamizi ili kubadilisha mwenendo wa ukuaji wa misamaha ya kodi. Maboresho yanayopendekezwa yatakuwa chini ya sheria zifuatazo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani;
(b) Sheria ya Kodi ya Mapato;
(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa;
(d) Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli;

(e) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa;
(f) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
(g) Matangazo ya Serikali yanayotoa Misamaha ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye matanki maalumu ya kuhifadhi maziwa *(heat insulated milk cooling tanks*) na vipipa vya alumini *(alminium jerry cans*) vya kukusanya maziwa ili kuhamasisha matumizi ya vyombo hivi kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi maziwa na hivyo kuongeza ubora wa maziwa na kipato kwa wananchi;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kilimo za kutayarisha mashamba, kulima, kupanda na kuvuna ili kupunguza gharama za uzalishaji kwenye kilimo. Hivi sasa pembejeo za kilimo na mbolea zinasamehewa kodi hii;

(iii) Kupanua wigo wa Msamaha Maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief)* unaotolewa kwenye maduka yasiyotoza kodi ya Jeshi la Ulinzi *(Defence Forces Duty Free Shops)* ili kujumuisha majeshi yote ya ulinzi na usalama *(Armed Forces).* Aidha, napendekeza kuweka utaratibu maalumu wa kusimamia msamaha ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutangaza katika Gazeti la Serikali orodha ya bidhaa zitakazohusika na msamaha huo ili kuzuia matumizi mabaya ya msamaha huo kwa vyombo husika;

(iv) Kupunguza wigo wa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief)* kwa asasi na mamlaka za maji safi na taka nchini ili msamaha huo uhusishe vifaa na huduma zitakazohusika katika ujenzi wa miundombinu ya maji safi na taka pekee. Hatua hii inalenga kuziba mwanya wa matumizi mabaya ya msamaha huo;

(v) Kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kukodi ndege (*Air Charter Services*), kwani huduma hizi hutolewa kibiashara kama huduma za kukodi vyombo vingine vya usafiri ambazo kisheria hulipiwa kodi;

(vi) Kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chai na kahawa iliyozalishwa na kusindikwa hapa nchini ili kuleta usawa na mazao mengine yaliyosindikwa ambayo hutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hivi sasa mazao yote ambayo hayajasindikwa hayatozwi kodi hii;

(vii) Kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine za elektroniki za kutunza kumbukumbu za mauzo *(Electronic Cash Register)* kwa kuwa mashine hizi hazitumiki tena kwa kazi hiyo na badala yake Mamlaka ya Mapato Tanzania wataanzisha, kwa awamu, matumizi ya mashine mpya za elektroniki za kutunza kumbukumbu za kodi *(Electronic Tax Register);*

(viii) Kuondoa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief)* kwenye mali ghafi na vifungashio kwa wazalishaji wa ndani wa dawa za binadamu kwa kuwa wazalishaji wa ndani wa dawa tayari wanapata unafuu

wa kodi kupitia Jedwali la Kwanza ambapo wanawajibika kulipa kodi na baadaye kurejeshewa. Ili kutoa muda wa kutosha kwa wazalishaji kujiandaa bila kuathiri uzalishaji, inapendekezwa hatua hii ianze kutekelezwa rasmi tarehe 1 Januari, 2010;

(ix) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upangishaji na ukodishaji wa nyumba na majengo *(leased buildings and serviced apartments)* isipokuwa zile zinazotolewa na Shirika la Nyumba la Taifa na Msajili wa Majengo. Hatua hii haitahusisha upangishaji wa nyumba na makazi ya kawaida ya wananchi kwa vile mapato wanayopata wapangishaji kutoka kwenye ada ya pango hayafikii kiwango cha usajili cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Registration Threshold*);

(x) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye muda wa maongezi kwenye simu kwa kutumia bei halisi inayooneshwa kwenye vocha badala ya bei nafuu anayotozwa muuzaji wa jumla. Lengo ni kuhuisha mapato yatokanayo na chanzo hiki cha kodi na kuziba mwanya wa ukwepaji kodi;

(xi) Kupunguza wigo wa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief)* kwa kampuni za madini, mafuta ya petroli na gesi ili msamaha huo uhusishe shughuli za utafiti na utafutaji pekee ambao hufanywa na mwekezaji kabla ya kuanza uzalishaji;

(xii) Kuondoa msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Special Relief)* kwa asasi zisizo za kiserikali *(NGOs)* na mashirika ya dini. Hatua hii itahusisha madhehebu yote ya dini ambayo ni pamoja na Waislamu, Wakristo, Wahindu, Mabohora na kadhalika. Hata hivyo, vifaa vya kiroho na ibada vitaendelea kupata msamaha wa kodi;

(xiii) Kufuta utaratibu wa sasa wa kutambua baadhi ya vifaa kama bidhaa za mitaji kwa baadhi ya wawekezaji kwa nia ya kuvipa unafuu wa kodi (*deemed capital goods*). Kwa mfano, wawekezaji katika sekta ya hoteli na utalii hutumia unafuu huu kuingiza vifaa kama mashuka, glasi, vijiko, uma na visu ambavyo hutambuliwa kama bidhaa za mitaji;

(xiv) Kupunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asimilia 20 ya mauzo hadi asilimia 18 ya mauzo ili kupunguza makali ya athari za msukosuko wa uchumi duniani. Punguzo hili linatarajiwa kujenga mazingira ya kuongeza kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari; na

(xv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upakiaji na upakuaji mizigo kwenye meli za hapa nchini kwa mizigo iliyotoka nje ya nchi na ambayo huduma ya kupakua mizigo kutoka kwenye meli iliyoleta mizigo kutoka nje ya nchi ilishatozwa kodi hii. Hatua hii inalenga kuhamasisha wafanyabiashara kushusha mizigo katika bandari zetu nyingine za Tanga na Mtwara na hivyo kupunguza msongamano wa meli na mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 45,078 milioni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 ya faida hadi asilimia 25 kwa makampuni yanayoorodheshwa katika soko la mitaji na kuuza angalau asilimia 30 ya hisa zake kwa wananchi ili kuhamasisha kampuni kujiorodhesha katika soko la mitaji na kuongeza umiliki wa wananchi kwenye hisa za kampuni. Hatua hii inazingatia maamuzi ya Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii ya Kodi ya Mapato itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 3,992 milioni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kuondoa msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya petroli kwa makampuni ya madini kwa kuwa Serikali inapoteza kiasi kikubwa cha mapato ya kodi kutokana na msamaha huu na hivyo kupunguza uwezo wake wa kutoa huduma. Msamaha huu hutolewa kupitia Tangazo la Serikali Namba 480 la Mwaka 2002;

(ii) Kutoza Ushuru wa Bidhaa katika huduma za simu za mkononi pale vocha au muda wa maongezi unapouzwa badala ya kusubiri hadi muda wa maongezi utumike; na

(iii) Kurekebisha kwa asilimia 7.5 viwango maalumu vya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zinazotozwa ushuru huu, isipokuwa zile za mafuta ya petroli. Marekebisho haya yamezingatia kiasi cha wastani wa mfumko wa bei. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo: Vinywaji baridi kutoka shilingi 54 kwa lita hadi shilingi 58 kwa lita; bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 194 kwa lita hadi shilingi 209 kwa lita; bia nyingine zote kutoka shilingi 329 kwa lita hadi shilingi 354 kwa lita; mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,053 kwa lita hadi shilingi 1,132 kwa lita; na vinywaji vikali kutoka shilingi 1,561 kwa lita hadi shilingi 1,678 kwa lita.

(iv) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 5,348 hadi shilingi 5,749 kwa sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 12,618 hadi shilingi 13,564 kwa sigara elfu moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 22,915 hadi shilingi 24,633 kwa sigara elfu moja;

(d) Tumbaku ambayo ipo tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 11,573 hadi shilingi 12,441 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa (*Cigar*) unabaki asilimia 30.

Hatua hizi katika Ushuru wa Bidhaa, kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 72,691 milioni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuondoa msamaha wa Ushuru wa Mafuta ya Petroli kwa mafuta yanayotumiwa na makampuni ya madini kwa kufuta Tangazo la Serikali Namba 99 la Mwaka 2005. Marekebisho haya yanahusu makampuni ya madini yatakayoingia mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Aidha, napendekeza Serikali ianze kufanya mazungumzo na makampuni ya madini ili kuondoa kipengele kinachohusu msamaha huu kwenye mikataba.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kupunguza kiwango cha ukomo cha kutoza ushuru wa mazao kutoka asilimia tano ya bei ya kuuza mazao shambani hadi asilimia tatu ili kupunguza makali ya athari za msukosuko wa uchumi duniani kwa wakulima nchini. Hata hivyo, napendekeza hatua hii ianze kutekelezwa mwaka wa fedha 2010/11 ili kutoa nafasi kwa Serikali za Mitaa kujiandaa kupata vyanzo mbadala vya mapato.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Tanzania ya kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha, yalijadiliwa pamoja na yale ya kutoka Kenya, Uganda na Rwanda katika kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kilichofanyika tarehe 20 Mei 2009, Nairobi Kenya. Katika kikao hicho, Mawaziri wa Fedha walikubaliana kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(i) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye matanki maalumu ya kuhifadhi maziwa (*heat insulated milk cooling tanks)*, kwa ajili ya sekta ya maziwa ili kuhamasisha matumizi ya vyombo hivi katika ukusanyaji na uhifadhi wa maziwa na hivyo kuongeza ubora na kipato kwa wananchi;

(ii) Tanzania kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambulika chini ya HS Codes 1001.90.20 na 1001.90.90 kwa muda wa mwaka mmoja kwa vile bado uzalishaji wa ngano katika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki haujaweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani;

(iii) Tanzania kuondoa Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 unaotozwa kwenye dawa za binadamu na kutoza asilimia sifuri kama ilivyo kwa nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni matumaini ya Serikali kwamba, hatua hii itawawezesha wananchi kupata dawa kwa bei nafuu;

(iv) Tanzania kuondoa Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 unaotozwa kwenye mafuta ghafi ya kula ya mawese *(Crude Palm Oil)* na kutoza asilimia sifuri kama ilivyo kwa nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii inalenga kuviweka viwanda vya mafuta vya hapa nchini katika nafasi nzuri ya kiushindani na vile vya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(v) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye vipuri vya viwanda, kwa kufuata utaratibu na vigezo maalumu vitakavyoandaliwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kushirikiana na nchi wanachama kwa nia ya kupunguza gharama za uzalishaji na kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Viwanda;

(vi) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye magari yaliyotengenezwa maalumu kwa ajili ya kubeba watalii ili kuhamasisha na kukuza biashara ya utalii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeagizwa kuandaa vigezo vitakavyotumika kutambua magari hayo;

(vii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye mitambo, vifaa na mali ghafi vinavyoagizwa na kampuni zilizosajiliwa kwa ajili ya utafiti, utafutaji na uendelezaji wa uchimbaji wa mafuta ya petroli na gesi. Msamaha huu hautahusisha magari;

(viii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye mali ghafi kwa ajili ya kutengeneza visodo na taulo za usafi za wanawake (*tampons and sanitary towels)* ili kuwawezesha kupata vifaa hivi vya usafi kwa bei nafuu;

(ix) Kuondoa Ushuru wa Forodha kwenye bamba la nyuzinyuzi za asibesto *(asbestos fibres)* zinazotambulika chini ya HS Codes 6812.80.00 na 6812.99.00 ambazo hutumika katika kutengeneza *brake linings* kwa kuwa mali ghafi hizi hazizalishwi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(x) Kuondoa Ushuru wa Forodha kwenye kamera maalumu za kupiga picha za filamu zinazotambulika chini ya HS Codes 8525.80.00 ili kuhamasisha sekta ya filamu kwa nia ya kuongeza ajira na kipato kwa vijana;

(xi) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye nguo za mitumba kutoka asilimia 45 au senti 30 za dola kwa kilo hadi asilimia 35 au senti 20 za dola kwa kilo kwa muda wa mwaka mmoja;

(xii) Kuongeza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye maziwa ya mtindi yanayotambulika chini ya HS Codes 0403.10.00 na 0403.90.00 kutoka asilimia 25 hadi asilimia 60 ili kulinda sekta ya maziwa dhidi ya ushindani mkubwa kutoka nje ya Jumuiya;

(xiii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye mali ghafi zinazotumiwa na viwanda vya kutengeneza karatasi. Aidha, Tanzania na Kenya zitawasilisha kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, orodha ya viwanda vya kutengeneza karatasi na mahitaji yao ya mali ghafi;

(xiv) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye magari ya mizigo ya angalau tani tano yanayotambulika chini ya HS Code 8704.22.90 toka asilimia 25 hadi asilimia 10 na kuondoa ushuru wa forodha kwa yale ya zaidi ya tani 20 yanayotambulika chini ya HS Code 8704.23.90 kwa muda wa mwaka mmoja, wakati utafiti unafanyika kuhakiki uwezo wa Kenya kuzalisha na kutosheleza mahitaji ya magari hayo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za usafirishaji na kuhamasisha uzalishaji; na

(xv) Kuondoa kodi kwenye nyuzi za kufuma vitambaa zisizo za pamba ili kupunguza gharama kwa wazalishaji ambao hutumia nyuzi hizi kwa ajili ya kuchanganya na nyuzi za pamba.

Hatua hizi katika Ushuru wa Forodha kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 23,622 milioni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufuta Matangazo ya Serikali 405 yanayotoa misamaha ya kodi kwa kampuni binafsi; asasi zisizo za kiserikali; taasisi za kidini; mashirika ya kimataifa na miradi ya Serikali iliyokwishakamilika ili kuziba mwanya wa kuvujisha mapato ya Serikali. Mengi ya matangazo haya yalitolewa katika kipindi cha mwaka 1964 na 2005 yamebainika kuwa na upungufu, ikiwemo kutokuwa na ukomo wa muda wa kutumika au kiasi kinachosamehewa kodi; na kutobainisha wazi kodi zinazosamehewa. Hata hivyo, ikitokea tangazo lililofutwa bado linahitajika, mhusika atashauriwa kuomba upya kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara Zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Aidha, ili kuinusuru sekta ya utalii katika kipindi hiki cha msukosuko wa uchumi duniani, inapendekezwa kupunguza viwango vya ada ya VISA na kuwa na kiwango kimoja cha dola hamsini.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2009, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/10, Serikali imepanga kupata jumla ya shilingi milioni 9,513,685 (trilioni 9.5). Kati ya kiasi hicho; mapato ya ndani ni Shilingi milioni 5,096,016 (trilioni 5.1) na mapato kutoka kwa wahisani ni shilingi milioni 3,181,948 (trilioni 3.2). Aidha, Serikali inategemea kupata shilingi bilioni 15, ikiwa ni salio kutokana na uuzaji wa hisa zake asilimia 21 katika Benki ya NMB. Serikali imepanga kukopa kiasi cha shilingi milioni 1,082,669 (trilioni 1.1) kutoka soko la ndani kwa ajili ya kugharimia Bajeti ya Serikali pamoja na kulipia hatifungani zitakazopevuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, matumizi ya Serikali yatakuwa shilingi milioni 9,513,685 (trilioni 9.5). Matumizi ya kawaida yatakuwa shilingi milioni 6,688.254 (trilioni 6.7). Matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi milioni 2,825,431 (trilioni 2.8). Katika matumizi ya maendeleo, kiasi cha shilingi milioni 1,857,403 (trilioni 1.9) zitatokana na fedha za wahisani kupitia miradi, pamoja na mifuko ya kisekta. Kiasi kilichobaki cha shilingi milioni 968,028 zitatokana na mikopo ya ndani pamoja na sehemu ya mchango wa wahisani kupitia misaada ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, sura ya bajeti inakuwa kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

| | | Shilingi Milioni | |
|---|---|---|---|
| A. | <u>Mapato</u><br>Mapato ya Ndani | | 5,096,016 |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 4,855,935 | |
| | (ii) Mapato yasiyo ya Kodi | 240,081 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| B. | Mapato ya Halmashauri | | 138,052 |
| C. | Mikopo na Misaada ya Nje | | 3,181,948 |
| | (i) Misaada na Mikopo ya Kibajeti | 1,193,909 | |
| | (ii) Misaada na Mikopo ya Miradi | 1,073,170 | |
| | (iii) Misaada na Mikopo ya Kisekta | 572,927 | |
| | (iv) MDRI/MCA(T) | 341,942 | |
| D. | Mikopo ya Ndani | | 1,082,669 |
| E. | Mapato ya Ubinafsishaji (salio la mauzo ya hisa NMB) | | 15,000 |
| | JUMLA YA MAPATO YOTE | | 9,513,685 |
| | Matumizi | | |
| F. | Matumizi ya Kawaida | | 6,688,254 |
| | (i) Deni la Taifa | 1,523,024 | |
| | (ii) Wizara | 3,476,243 | |
| | (iii) Mikoa | 123,013 | |
| | (iv) Halmashauri | 1,565,974 | |
| G. | Matumizi ya Maendeleo | | 2,825,431 |
| | | | |
| | JUMLA YA MATUMIZI YOTE | | 9,513,685 |

Mheshimiwa Spika, pamoja na msukosuko wa kifedha na kiuchumi duniani, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu pamoja na Wananchi kwa ujumla kwamba, Bajeti ya Mwaka 2009/10 itatekelezeka kama ilivyopangwa. Kwa kuzingatia mikakati tuliyojiwekea, tutahakikisha kwamba, msukumo unawekwa kwenye kilimo kwanza na kusisitiza matumizi ya fedha za umma katika maeneo yenye kuleta tija. Kama nilivyoeleza hapo awali, athari za msukosuko wa kifedha na kiuchumi zilizojitokeza, zinatarajiwa kupunguza kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2009; hivyo ni lazima juhudi za makusudi zichukuliwe kukabiliana na athari hizo.

Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, inalenga uchumi kukua kwa zaidi ya asilimia nane ili kupunguza umaskini na kuwa nchi yenye uchumi wa kiwango cha kati cha mapato na maisha bora. Kwa hiyo, unahitajika umakini zaidi katika matumizi ya rasilimali tulizonazo ili kuweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa haraka zaidi. Hivyo, kila mmoja wetu anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli halali za uzalishaji mali kwa nafasi yake. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia kwa caribú, viashiria muhimu vya uchumi ili kuhakikisha kwamba, athari zozote zitakazojitokeza zinatafutiwa mbinu za kuzikabili kabla hazijasababisha madhara zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ni dhahiri makofi hayo yanampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa Hotuba ya Bajeti na kuipongeza Serikali ambayo imewezesha Bajeti hii ichukue mfumo huo iliyouchukua.

Sasa niwakumbushe tu, safari hii kazi nzuri inaendelea kufanywa na Serikali; Kitabu cha *Revenue Estimate* kipo tayari sio kama mwaka jana. Kwa hiyo, Kitabu Namba Moja kitagawiwa hivi punde, kipo tayari kimewekwa mezani, Waheshimiwa Wabunge mtakipata ili mnapojadili pia muweze kuona hatua zilizopo katika *Financial Statement* na *Revenue Estimates.*

Nadhani asubuhi mmepokea mpangilio wa jinsi ambavyo Wizara zitawasilisha makadirio yake, zipo kwenye karatasi ya rangi ya njano. Kabla sijaendelea na mambo mengine, nadhani ni vyema tuwatambue baadhi ya watu mashuhuri ambao tunao hapa katika kusikiliza Hotuba ya Bajeti ndani ya Ukumbi huu.

Kwanza, kwa heshima na taadhima, namwomba Mama Tunu Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu asimame; ahsante sana mama. Vilevile Katibu Mkuu Kiongozi yuko hapa, Ndugu Luhanjo; pia tunae Mkuu wa Mabalozi *(Dean of Diplomatic Corps)* Balozi Juma Mpango wa DRC yule pale.

Ningependa muelewe pia kwamba, kutokana na nafasi finyu, Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha nchi mbalimbali zinazowakilishwa hapa nchini, wako kwenye *Gallery* mkono wa kulia. *I request that Members of the Diplomatic Corps and Ambassadors represented here in Tanzania, who are in the Gallery on my right hand, please stand up to be acknowledged;* wale pale ahsante sana. *We sincerely value your contribution as development partners. Thanks very much. (Makofi)*

Wapo Wakuu wa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, Jeshi la Ulinzi; General Mwamunyange yule pale; IGP Said Mwema yule pale, DGIS Othman yule pale; na Kamishna Mkuu wa Magereza, Ndugu Nanyaro. *(Makofi)*

Tunae Mstahiki Meya wa Dodoma, ahsante sana Mstahiki; mkono wa kushoto pale Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Jaji Makame yule pale; Tukikutaja Mheshimiwa Jaji, tunapata joto kidogo maana yake lah! wewe ndio utaamua hatima yetu. *(Makofi)*

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Ludovic Utoh; huyu amesaidia sana kuleta mapinduzi makubwa katika ukaguzi, tunampongeza. Sisi Wabunge tunakupenda sana, nadhani wananchi pia waelewe kazi yako. *(Makofi)*

Yupo Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Benno Ndulu. *(Makofi)*

Naibu Gavana wa *BOT* hakutajwa lakini asubuhi tulitaja wawili nadhani Naibu Gavana; ahsante sana. *(Makofi)*

Msajili wa Vyama vya Siasa, Mheshimiwa Tendwa, ahsante sana. Kamishna Mkuu wa *TRA*, Ndugu Kitilya yule pale, hongera sana kwa kazi nzuri, pamoja na misukosuko mmefanya jitihada kubwa sana. Kapteni John Barongo, Katibu Mkuu wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, ahsante sana.

Mama Mkulo, sijui kwa nini huyu hatajwi jina lake, lakini inawezekana ndio siri za Hazina hizi. Mrs Mkulo tafadhali, mke wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi*)

Mtuwie radhi wengine sio kwamba si mashuhuri, lakini nadhani muda pia hauruhusu kuweza kuwatambua wote. Ooh! Katibu wa Bunge Mstaafu, Ndugu Damiani Foka yupo! Ahsante sana. *(Makofi)*

Ndugu Damian Foka, hatuwezi kukusahau; wewe ndiye uliyeweka misingi inayowezesha Bunge hili kuendelea kwa nguvu kama linavyoendelea sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha imekwisha tolewa na imeungwa mkono, lakini kama ulivyo utaratibu wetu na mkizingatia uzito wa hoja yenyewe sio ya kuiparamia tu mara ikishatolewa basi unakwenda tu unaanza kuchangia; tuna utaratibu kwamba, hoja hiyo mtaanza kuichangia Siku ya Jumatatu, baada ya maswali. Naomba niwakumbushe tu kwamba, kesho kutakuwa na kipindi cha maswali.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 12 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*